SUPA JACKPOT
TZS. 1,090,583,531
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 19

**MTOTO** wa Museveni atangaza kugombea urais kumrithi baba


Ukurasa 12
Machimbo mapya ya graphite kupaisha uchumi Ruangwa, pia zawadi ajira 1600
Ukurasa 13
Wanaolawiti na kunajisi watoto, adhabu iliyopo leo bado haitoshi
Ukurasa 14
BUFE
IJUMAA MACHI 17, 2023
Nipashe
MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA
Mbunifu Rose Urio : Ahsante mama kukaribisha vazi 'Batiki Mshumaa'
MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA
Dk. Mpango na Waziri Mwigulu walivyotoa ushuhuda kikaoni Doha makubwa ya nchini

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Machi 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581252


www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kilio Toto Afya Kadi chatikisa



**WADAU** waonya wengi kukosa matibabu kisa... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akivalishwa nishani ya heshima kutoka kwa mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kabla ya kuzungumza na waandishi wa habari jijini Pretoria jana, katika ziara yake ya kiserikali nchini humo. **PICHA: IKULU**

## Samia apewa nishani uongozi bora

UKURASA 2

UKURASA WA 2

### MAHAKAMA YAZUIA MKUTANO WA CWT

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Kazi Dodoma imezuia mkutano wa uchaguzi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) uliopangwa kufanyika leo jijini Tanga.
Hatua hiyo inatokana na kufunguliwa kwa kesi ya msingi kupinga kufutwa...

UKURASA WA 3

### MSHTAKIWA AIOMBA MAHAKAMA AKUTANE NA MKE WAKE

MSHTAKIWA Said Matwiko pamoja na Kocha wa makipa wa Klabu ya Soka ya Simba, Mwalami Sultan, wanaoshtakiwa kwa kusafirisha dawa za kulevya ameiomba mahakama akutane...

## Mbowe: Vyama vya siasa visiwe sababu kutugawa

UKURASA 3

UKURASA WA 4

### MUHIMBILI KUANZA KUPANDIKIZA INI

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH), imesema iko kwenye hatua nzuri za maandalizi ya kuanza kufanya upandikizaji wa ini ifikapo mwaka 2025 ili kuwapunguzia...



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Timotheo Mzava (kushoto), akiwa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (wa pili kushoto), na wajumbe wa kamati hiyo, wakimwangalia kobe mzee mwenye umri wa miaka 160 katika Makumbusho ya Elimu ya Viumbe Hai jijini Arusha jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

**MICHEZO** YANGA : TUTAIDUWAZA US MONASTIR JUMAPILI UK. 24

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA

# Mahakama yazuia mkutano wa CWT

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Kazi Dodoma imezuia mkutano wa uchaguzi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) uliopangwa kufanyika leo jijini Tanga.

Hatua hiyo inatokana na kufunguliwa kwa kesi ya msingi kupinga kufutwa uanachama kwa waliokuwa viongozi wa chama hicho.

Viongozi hao ni aliyekuwa Katibu Mkuu, Deus Seif na Mtunza Hazina, Abubakar Allawi, ambao Desemba, mwaka jana, mkutano mkuu wa chama hicho uliazimia kuwavua uanachama huku wakiwa wanasubiri uamuzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kuhusu rufani ya kesi ya jinai. Zuio la mkutano huo lilitolewa jana na Jaji Gerson Mdemu baada ya Seif na Allawi kuwasilisha maombi ya kuzuia uchaguzi wa nafasi hizo.

Akizungumza nje ya mahakama baada ya uamuzi huo, wakili upande wa waleta maombi, Nashon Nkungu, alidai uamuzi huo unatoa nafasi ya kusikilizwa kwa kesi ya msingi ya waleta maombi ya kuiomba Mahakama Kuu kutoa tafsiri ya mkutano mkuu wa nusu muhula wa CWT kuwajadili na kuwafuta uanachama wakati wakiwa na kesi mahakamani.

"Sababu iliyosababisha waleta maombi waombe zuio la mahakama na kupewa ni uwapo wa kesi ya kujadili uhalali wa wao kuondolewa kama wanachama na kuondolewa kwenye nafasi za uongozi walizokuwa wakizitumikia," alisema.

Mkutano mkuu huo wa nusu muhula, uliazimia kuwafuta uanachama Seif na Allawi kutokana na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, baada ya kupatikana na hatia ya kutumia vibaya madaraka kwa kuchepusha Sh. milioni 13.9 ambazo ni mali ya CWT, hivyo kukosa sifa ya kuwa viongozi na wanachama.

Hata hivyo, wakati mkutano huo ukiazimia hayo, watuhumiwa hao walikuwa wamekata rufani wakisubiri hukumu kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam. Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilitoa uamuzi kuhusu rufani hiyo ambayo Seif na mwenzake walishinda baada ya ushahidi uliotolewa kutowatia hatiani.



Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, akipiga makofi baada ya kuzindua mradi wa ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji kati ya Makongo Juu na mji wa Bagamoyo, eneo la Tegeta A mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (wa tatu kulia) na (wa nne kulia) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Jenerali mstaafu Devis Mwamunyange. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kilio cha bima Toto Afya Kadi chatikisa

**Na Waandishi Wetu**

WADAU mbalimbali wa masuala ya afya, wamezidi kusema hatua ya serikali kufanya maboresho katika bima ya afya kwa kuondoa mfumo wa Toto Afya Kadi utasababisha athari kutokana na wazazi wengi kutokuwa na uwezo kifedha.

Aidha, wameshauri kuwa ni vyema serikali ikarejesha bima hiyo kwa watoto ambayo malipo yake ni Sh. 50,400 ili kuwezesha kundi hilo kupata huduma za matibabu kwa unafuu na kwa urahisi.

Mwanzoni mwa wiki, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ulifanya maboresho ya utaratibu wa usajili na huduma kwa watoto waliokuwa wanasajiliwa kupitia Toto Afya Kadi kwa kile ilichosema lengo ni kuwafikia watoto wengi ambao wako nje ya huduma.

Kutokana na maboresho hayo, wazazi au walezi wanatakiwa kuwasajili watoto kama wategemezi wao kwenye bima ya afya au kupitia shule wanazosoma, hatua ambayo wadau wengi wameonyesha kutoridhishwa nayo.

Jana, Taasisi ya Asma Mwinyi kwa kushirikiana na Bigger Heart Zanzibar, iliwatembelea watoto wanaopatiwa matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na kuwapatia vifaa mbalimbali vya kuchezea kwa lengo la kuwafariji.

Baada ya kupokea zawadi hizo, Mkuu wa Kitengo cha Ustawi wa Jamii wa JKCI, Asha Salum, alishauri kuwa ni vyema mfumo wa Afya Toto Kadi ukabaki kama awali ili kuwasaidia wazazi wenye kipato cha chini kumudu gharama na watoto kupata matibabu.

Alibainisha kuwa wanakutana na changamoto mbalimbali kwa kuwa wanapokea wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali na kwamba wengi hawana uwezo wa kumudu gharama za matibabu.

"Hili la bima ya watoto lingebaki kama awali kwa sababu kuna mzazi anashindwa kuikata hiyo bima mpaka tunaomba msaada kwa mtu mwingine. Sasa unaposema mzazi akate bima ambayo ni kubwa na mtoto aingizwe watoto wengi watakosa huduma," alisema.

"Watarudi kwenye msamaha kiasi kwamba taasisi zitashindwa kujiendesha, kwa ushauri wetu tunaomba bima za watoto zibaki kama zilivyo, wazazi watafute utaratibu mwingine, kwa sababu tutarudi huduma zitakuwa zimezorota sana," alishauri.

Daktari wa watoto wa JKCI, Dk. Zawadi Edward, alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo ni baadhi ya wazazi kushindwa kumudu gharama za upasuaji kwa watoto na kwamba bima ya afya inawasaidia licha ya baadhi yao kushindwa kulipia.

**WADAU WAKOLEZA**

Mmoja wa wadau wa masuala ya bima, Anselm Anselm, alishauri elimu ielekezwe kwa wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya kabla ya kutangaza vifurushi ambavyo vinazua mijadala.

Kuhusu Toto Afya Kadi, alisema: "NHIF ingeelemisha kwanza wananchi na kisha gharama ziwekwe. Kwa vyovyote vile, watoto na wazee ndio huumwa sana, ingekuwa kila mtoto anapozaliwa anaanza kuchangiwa bima ya afya." Salima Suleiman, mkazi wa Ilala, Dar es Salaam, alisema bima ya Toto Afya ilipaswa kubaki kwa kuwa inasaidia watoto wengi hasa wale ambao wazazi wao hawapo kwenye ajira rasmi.

"Naona NHIF hawakuzingatia mahitaji ya jamii ya Watanzania walio wengi. Malengo ya dunia ni kupunguza vifo vya mama na mtoto ifikapo 2030, itakuwa ndoto. Taifa lisilozingatia afya na tiba ya watu wake ni ngumu kusonga mbele," alisema.

**Imeandikwa na Maulid Mmbaga na Christina Mwakangale**

# Rais Samia atunukiwa nishani ya uongozi bora

**Na Halfani Chusi**

RAIS Samia Suluhu Hassan jana alitunukiwa nishani ya uongozi na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kutokana na kutambua mchango wake kama kiongozi mwanamke aliyewaunganisha watu na kudumisha uhusiano baina ya nchi hizo.

Nishani hiyo ilitolewa jana jijini Pretoria, Afrika Kusini, katika hafla iliyoambatana na utoaji saini mikataba mbalimbali ya ushirikiano baina ya Tanzania na Afrika Kusini.

Rais Samia aliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye mazungumzo na mwenyeji wake na alishiriki Jukwaa la Biashara, kufanya mazungumzo ya pamoja kwa mustakabali wa nchi zao na kuzungumza na kujibu maswali ya waandishi wa habari.

Pia Rais Ramaphosa alimtembeza Rais Samia kwenye maeneo mbalimbali ya Ikulu ya Afrika Kusini na majengo ya mji wa Pretoria katika ziara hiyo ya kikazi.

Rais Samia pia alikagua gwaride la heshima baada ya kuwasili katika viwanja vya mapokezi ya uongozi eneo la majengo ya Union, Pretoria.

Akijibu maswali ya waandishi wa habari, Rais Samia alisema urafiki kati ya Tanzania na Afrika Kusini, hautakufa kutokana na historia yake. Alisema ziara hiyo ni nafasi adimu kwake kuelezea mambo anayotamani Tanzania na nchi hiyo zishirikiane ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Ziara hii inaonyesha ni kwa jinsi gani tunatamani kuona maendeleo ya watu katika nchi tunazoziongoza kwenye sekta mbalimbali. Nina furaha sana nimepewa nishani ya heshima ya kutambua mchango wangu.

"Katika kuisaidia Afrika Kusini kupambana na ubaguzi wa rangi na mchango wangu kama Rais wa kwanza mwanamke Tanzania, hii nishani si kwa ajili yangu tu bali kwa Watanzania wote," alisema. Aliyataja baadhi ya mambo waliyojadiliana na Rais Ramaphosa kuwa ni pamoja na siasa safi huku akitolea mfano alivyohudhuria kwenye mkutano siku ya wanawake dunia ulioandaliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), amani na upendo pamoja na kujadiliana kwa pamoja namna ya kulinda utamaduni wetu.

"Pia tuligusia kidogo kwenye elimu na masuala ya utamaduni na michezo na kuna mpango wa kuzindua maonyesho ya utamaduni wetu kati ya hizi nchi mbili, hii itatoa nafasi kwa nchi zote mbili kutambulisha na kuenzi utamaduni wetu.

"Lakini tumekubaliana kuanzisha shule za kufundisha Kiswahili hapa Afrika Kusini, hii itasaidia kueneza lugha yetu," alisema.

Rais Ramaphosa alimshukuru Rais Samia na viongozi alioambatana nao katika ziara hiyo huku akiahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania kwenye nyanja mbalimbali.

## HABARI KITAIFA



Mafundi ujenzi wakichimba msingi kwa ajili ya kujenga uzio ili kutenganisha makaburi ya Mlandege na eneo la wafanyabiashara wadogo machinga, mjini Iringa jana, baada ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM wa mkoa huo, Salim Abri Asas kutoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya eneo hilo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mshtakiwa aomba mahakama akutane na mke malezi watoto

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Said Matwiko pamoja na Kocha wa makipa wa Klabu ya Soka ya Simba, Mwalami Sultan, wanaoshtakiwa kwa kusafirisha dawa za kulevya ameiomba mahakama akutane na mshtakiwa mwenzake Sarah Eliud ambaye ni mke wake ili wazungumze kuhusu malezi ya watoto wao.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mmiliki wa Kituo cha Soka cha Kambiasso Sports Academy, Kambi Seif, Maulid Mzungu, Said Matwiko, John John na Sarah Eliud.

Matwiko alitoa ombi hilo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ikiendeshwa kwa njia ya mtandao 'Video Conference', washtakiwa wakiwa mahabusu.

Alidai kuwa tangu walipokuwa mahabusu hawajaonana kuzungumza kuhusu malezi ya watoto wao na anaiomba mahakama iwasaidie akutane na mke wake Sarah ili wapange jinsi watoto wao watakavyoishi.

Baada ya ombi hilo, hakimu alipanga Machi 30, 2023 kwa ajili ya kutajwa na pia aliagiza siku hiyo washtakiwa waletwe mahakamani ili kesi isiendeshwe kwa njia ya mtandao.

Awali, Wakili wa Serikali Caroline Matemu, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na aliomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi.

Mara ya mwisho kutajwa kwa kesi hiyo, Sarah aliiomba mahakama kuharakishwa kukamilika kwa upelelezi wa kesi hiyo kwa sababu yupo gerezani na hajui watoto wake wanalelewaje.

Alidai kuwa yupo gerezani hajui watoto wake wanaendeleaje na wanalelewaje na kuomba upande wa mashtaka uharakishe kukamilika kwa upelelezi.

Sarah alidai wapo ndugu ambao wanakwenda kumtembelea, lakini hajui watoto wake wanalelewa katika mazingira gani, "Basi vumilia hadi upelelezi utakapokamilika," alisema Hakimu Mrio.

Ilidaiwa kuwa Oktoba 27, 2022 katika eneo la Kivule, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 27.10 za dawa za kulevya aina ya herione.

Katika shtaka la pili ilidaiwa Novemba 4, 2022 huko Kamegele katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Hata hivyo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu kwa kuwa Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

# Mbowe: Vyama vya siasa visiwe chanzo kutugawa

**Na Mathias Marwa,** SERENGETI

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amewataka wananchi kutanguliza uzalendo kwa taifa lao na kuweka mbele zaidi mshikamano kitaifa badala ya kukumbatia vyama vya siasa vinavyowagawa na kuwafanya waendelee kuwa maskini huku viongozi wachache wakinufaika na mapato ya rasilimali za nchi.

Alitoa kauli hiyo juzi, wakati akihutubia wananchi mjini Mugumu wilayani Serengeti, mkoani Mara kuwa wakati umefika kuwataka wananchi kuwa kitu kimoja bila kujali itikadi za vyama vyao.

Aidha, suala la kudai Katiba mpya itakayojali haki, uhuru, usawa na demokrasia kwa watu wote litafanikiwa endapo wananchi watapaza sauti zao bila kujali itikadi za vyama vyao ili kupata itakayoharakisha maendeleo kwa wote.

Alisema ameishaongea na Rais Samia Suluhu na kumweleza kuwa nchi inakokwenda siko na kwamba ukombozi pekee wa Watanzania ni Katiba mpya.

Alibainisha kuwa Katiba iliyopo itaendelea kuwalinda wakubwa waendelee kutenda wanayotaka wao, lakini haimsaidii mwananchi mwingine kustawi kijamii, kisiasa na kiuchumi.

"Katika hili tuungane pamoja tuache itikadi za kisiasa turekebishe Katiba kwa ushirikiano mkubwa ili tuokoe jamii yetu," alisema.

Kuhusu elimu alisema mfumo uliopo haulengi kumfanya mwananchi ajitambue sawasawa na mataifa mengine akitokea mfano Kenya, Misri na Africa Kusini ili kuendana na sayansi na teknolojia bali ni mfumo wa kuwagawa katika makundi mawili ya maskini watawaliwa na matajiri watawala.

Katika hatua nyingine Mbowe aliitaka serikali kuwaonea huruma wananchi waishio karibu na hifadhi hususani kipindi wanapovamiwa na wanyamapori na kuwaua pamoja na mifugo yao huku wakijaribu kujihami dhidi ya wanyama hao hukamatwa na kutaifishwa hali inayozidi kuchochea umaskini.

Naye aliyewahi kuwa Mbunge wa Arusha kwa tiketi ya CHADEMA, Godbless Lema, alisema amerudi nchini kutoka uhamishoni nchini Canada ambako alilazimika kukimbilia ili kunusuru roho yake.

Lema alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameweka mambo vizuri sasa yupo na wanapigania marekebisho ya Katiba iwakomboe wananchi.

John Heche aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime vijijini, alisema Katiba mpya ikipatikana itaboresha maisha ya wananchi na kupunguza umaskini kwa wananchi waishio karibu na hifadhi za wanyamapori zinaongoza duniani pamoja na madini yasiyoisha.

Heche alisema, mito, milima na mabonde vinatosha kuajiri watu wengi na kupunguza umaskini ikiwa Katiba itakuwa na mwelekeo wa kuonesha njia chini ya watu makini.

Ziara ya viongozi wa juu wa CHADEMA katika maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa Victoria iliyotarajiwa kuendelea katika visiwa vya Ukerewe, imesitishwa kutokana na kifo cha Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Sylvester Masinde, kilichotokea juzi katika Hospitali ya Rufani ya Bugando.





Mkurugenzi wa Taasisi ya Al-hikma, Shekhe Nurdin Kishik, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mashindano ya Quraan Kitaifa Afrika na ya Dunia, yanayotarajiwa kufanyika Septemba 2 na 16 mwaka huu. Kushoto ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Aisha Sururu, Aisha Sururu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Muhimbili kuanza kupandikiza ini

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH), imesema iko kwenye hatua nzuri za maandalizi ya kuanza kufanya upandikizaji wa ini ifikapo mwaka 2025 ili kuwapunguzia gharama wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi.

Hatua hiyo, kwa mujibu wa MNH, imefikiwa baada ya mafanikio makubwa kwenye huduma ya upasuaji wa ini, upandikizaji wa vifaa vya kusikia na figo kwa watu 100.

Daktari Bingwa wa upasuaji wa mfumo wa chakula na ini wa hospitali hiyo, Ally Mwanga, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akizungumzia mkutano wa kimataifa wa madaktari wa ini unaoanza leo.

Alisema huduma zote za ugonjwa wa ini kuanzia upasuaji, dawa na tiba shufwaa (chemotherapy) zinapatikana nchini na kwamba wameshafanya upasuaji wa ini kwa mafanikio makubwa sana.

Zamani, alisema kulikuwa na wataalamu wachache kiasi kwamba mtu aliyepata ugonjwa wa saratani ya ini ilionekana kama amepata tiketi ya kifo lakini kwa sasa hali imekuwa tofauti.

Dk. Manga Alisema MNH ilianza kufanya upasuaji wa ini mwaka 2020 na imepata mafanikio makubwa sana ndiyo sababu imepata uthubutu wa kuelekea kwenye upandikizaji wa ini.

"Hatua ya kwanza kuelekea kwenye upandikizaji wa ini ni kumudu upasuaji wa ini. Sasa tumeshafanikiwa kwa zaidi ya asilimia 70 kwa hiyo kwenye mipango yetu ni kufanya upandikizaji wa ini ifikapo mwaka 2025," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Manga, ili kufikia hatua ya upandikizaji wa ini kuna hatua nyingi za kupitia ikiwemo za kitaalamu na kuelimisha umma kuhusu ugonjwa huo kwani baadhi hawafahamu.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa MNH, Dk. John Rwegasha, alisema maandalizi yote ya kitaalamu, miundombinu na rasilimali fedha kuelekea kwenye upandikizaji wa ini yameshafanyika na imebaki hatua ndogo.

Alisema upandikizaji wa viungo vyovyote vya binadamu unagharama kubwa akitolea mfano wa watu wanaopandikiza vifaa vya usiku kuwa mgonjwa gharama yake ni hadi Sh. milioni 40.

Alitolea mfano mwingine kuwa upandikizaji wa figo kwa mgonjwa mmoja hapa nchini unafikia hadi Sh. milioni 20 na kwamba tayari wameshafanikiwa kupandikiza figo kwa watu 100.

Alisema wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi kwa ajili ya upandikizaji wa ini, wamekuwa wakilazimika kutoa zaidi ya Sh. milioni 50, hivyo kupatikana huduma hiyo nchini kutawapunguzia mzigo huo.

"Upandikizaji wa ini unahitaji miundombinu ya kisasa sana. Kwa mfano ndani ya hospitali unahitajika uwe na maabara inayojitosheleza vizuri na upatikanaji wa damu wa uhakika kwa sababu mgonjwa mmoja tu ili afanyiwe upasuaji wa ini anahitaji chupa 26 za damu kwa sababu upasuaji wa aina hiyo unaweza kuchukua hadi saa 24," alisema Dk. Rwegasha.

"Hawa mabingwa wa upasuaji wanasimama muda wote wa upasuaji kwa hiyo damu salama lazima nayo iwe kwenye mazingira salama. Lazima chumba cha uangalizi maalum (ICU) kiwe bora sana ili usipoteze mgonjwa kwa sababu anakuwa kwenye hali mbaya," aliongeza.

Daktari Bingwa huyo alisema kuna umuhimu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu utaratibu wa utoaji wa viungo kwani baadhi yao wamekuwa wakipiga simu wakitaka kutoa figo ili wapate fedha.

Alisema serikali inaandaa muswada kwa ajili ya kupelekwa bungeni utakaohusu namna ya utoaji wa viungo vya binadamu kwenda kwa mtu mwingine ili kuzuia utoaji holela.

"Hata mimi nimepata changamoto hiyo mtu anapiga simu na wengine wanakuja hospitali mtu anasema nina shida nyumbani naomba kuuza figo yangu. Sasa tusipodhibiti hali hii watu watakuwa wanachanwa chanwa na kutolewa viungo ndiyo maana hivi vitu vinahitaji sheria na miongozo," alisema

Alisema MNH iliamua kuanza kwa hatua moja moja na walianza kwa upandikizaji wa vifaa vya kusikia na upandikizaji wa figo ambavyo vyote hivyo wamevifanya kwa mafanikio makubwa.

"Tulipotoka kwenye upandikizaji wa vifaa vya kusikia tukaenda kwenye hatua ya upandikizaji wa figo kwa hiyo mazingira ya upandikizaji wa figo yanafanana na ya upandikizaji wa ini ingawa rasilimali zinaweza kutofautiana kidogo," alisema Dk. Rwegasha.

# Wadau washauri maboresho mazingira uwekezaji nishati

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa nishati ya jua nchini, wameishauri serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji wa teknolojia ya nishati jadidifu, ikiwamo kuweka sera itakayosimamia utekelezwaji wake, ili iwanufaishe watu wengi hasa wenye kipato cha chini.

Aidha, wameishauri teknolojia hiyo inakuwa kwenye ubora kutokana na kujitokeza baadhi ya changamoto na kuleta usumbufu kwa watumiaji, ikiwamo vifaa kuwa feki na kusababisha kudumu kwa muda mfupi.

Kauli hiyo imekuja ikiwa ni wiki moja tangu Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, aliposema Tanzania imeweka kipaumbele uwekezaji kwenye maeneo muhimu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo nishati ya jua na upepo katika Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea (LDCs) uliofanyika Doha nchini Qatar, Machi 4 hadi 9, mwaka huu.

Kupitia mkutano huo taasisi mbalimbali zinazotoa teknolojia hiyo, zilijitokeza kutaka ubia na nchi zinazoendelea ili kuipeleka, ikiwamo kampuni inayosambaza umeme wa jua Husk Power ya nchini Marekani kutangaza nia ya kushirikiana na nchi za jangwa la Sahara kupeleka nishati hiyo katika ngazi ya gridi ndogo.

Mjiolojia na Mtaalamu wa Maliasili za Nishati na Madini, John Bosco, alisema Tanzania ina nia njema na nishati za kutosha kuwekeza katika umeme wa jua na upepo isipokuwa kutokuwa na sera ya nishati jadidifu kunakorudisha nyuma maendeleo ya teknolojia hiyo.

Alisema ili suala hilo lifanikiwe serikali haina budi kufanya mabadiliko makubwa mifumo ya kitaasisi na kisheria katika uwekezaji, ikiwamo kuwa na sheria inayojitegemea inayosimamia uwekezaji wa nishati ya jua na umeme kama ilivyo kwenye mafuta na gesi, ili kufanikisha kuwapo na umeme wa jua katika ngazi ya gridi ya taifa. "Mfano ndani ya TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) imeundwa Kampuni Tanzu ya Geothermal inayoshughulikia nishati mbadala, lakini hakuna sheria inayoongoza utekelezaji wake, ipo sheria ya jumla lakini kila nishati hapo ina utofauti wake kwa hiyo inahitaji kuwa na sheria kuongoza utekelezaji wake," alisema Bosco.

Mwenyekiti wa Chama cha Nishati Jadidifu Tanzania (TAREA), Mhandisi Prosper Magali, alisema sera na sheria rafiki itasaidia kuwabana wawekezaji wa nishati hiyo ambao baadhi yao wanaleta teknolojia ambayo haijakamilika na kuwaachia mzigo wabia wa ndani kutafuta vifaa vilivyokosekana hali inayochangia huduma hiyo kuwa ghali.

"Hali iliyopo sasa ni kuwa mwekezaji anakuja na teknolojia ikiwa na vifaa nusu, inakubidi wewe unayeichukua uhangaike kwenda kutafuta baadhi ya vifaa kama vile paneli ambavyo vingi vipo chini ya kiwango, lakini kama ikija ikiwa imekamilika baadhi ya gharama zinapungua," alisema Magali.

Mmoja wa watumiaji wa nishati hiyo, Peter Kayanda, alisema moja ya changamoto wanayokutana nayo gharama ya kuunganishwa na umeme huo kuwa kubwa na vifaa kuwa feki na kulazimika kutumia pesa ya ziada kununua vifaa hivyo baada ya muda mfupi ya matumizi. "Tunaomba serikali iwabane hawa wanaotuletea hii teknolojia watuletee vifaa vilivyokuwa na ubora wa juu, hapa ninapokwambia nimeshabadilisha vifaa mara ya tatu sasa, vinaharibika kwa muda mfupi inakuwa ni mzigo kwetu," alisema.

Sera ya Nishati ya mwaka 2015 imesisitiza kuweka juhudi katika kuendeleza sekta ya nishati jadidifu mpaka kufikia asilimia 50 mwaka 2025, ili kuchochea upatikanaji wa nishati ya uzalishaji nchini.

Rais Samia Suluhu Hassan alipohutubia Mkutano wa 27 wa Kimataifa wa Tabianchi (COP27), uliofanyika Sharm el-Sheikh nchini Misri Novemba, mwaka jana, alisema pamoja na mambo mengine Tanzania itaongeza matumizi ya nishati jadidifu kwa asilimia 80 ifikapo mwaka 2025.

Aidha, Waziri wa Nishati, Januari Makamba, alipokuwa akisoma mipango ya utekelezaji wa bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2022/23 mapema mwaka jana, aliwaambia wabunge kuwa miongoni mwa vipaumbele vya bajeti hiyo ni utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu.

# China yarejesha usafiri watalii kwa nchi 60 ikiwamo Tanzania

**Na Mwandishi Maalumu**

WIZARA ya Utamaduni na Utalii ya China imetangaza kuanzia Jumatano wiki hii, imerejesha usafiri wa nje wa makundi ya watalii katika nchi na maeneo 40, na kufanya nchi na maeneo kwenye orodha hiyo kuwa 60.

Kwa mujibu wa tovuti ya gazeti la umma la nchini humo, hilo ni kundi la pili la nchi na maeneo kwenye mpango wa majaribio wa kurejesha usafiri wa nje wa makundi ya watalii baada ya nchi hiyo kurahisisha sera za kudhibiti UVIKO-19.

Taarifa hiyo inasema, mashirika ya utalii na tovuti za utalii zinaruhusiwa kuuza na kutembeza bidhaa na huduma zikiwamo za hoteli, tiketi za ndege na bidhaa nyingine za utalii wa makundi za nchi na maeneo hayo 40.

Nchi hizo zimetajwa kuwa Nepal, Brunei, Vietnam, Mongolia, Iran, Jordan, Tanzania, Namibia, Mauritius, Zimbabwe na Uganda.

Zingine ni Zambia, Senegal, Kazakhstan, Uzbekistan, Georgia, Azerbaijan, Armenia, Serbia, Croatia, Ufaransa, Ugiriki, Hispania, Iceland, Albania, Italy, Denmark na Ureno.

Vile vile zimo Slovenia, Vanuatu, Tonga, Samoa, Brazil, Chile, Uruguay, Panama, Jamhuri ya Dominican, El Salvador, Dominica na Visiwa vya Bahama.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya uendeshaji wa Akaunti ya Dhamana ya Bima iliyoandaliwa na Benki ya CRDB na TIRA, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PAC yataja mbinu kupunguza ajali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imesema iwapo kila mmoja atazingatia sheria, alama za usalama barabarani na taratibu zilizowekwa hakutakuwa na ajali zinazosababisha vifo kwa Watanzania.

Hayo yamesemwa na Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japheth Hasunga, baada ya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo barabara ya Njombe kwenda Makete yenye urefu wa kilomita 107 iliyojengwa kwa kugawanywa katika sehemu kuu mbili, ya kwanza kutoka Njombe - Moronga yenye urefu wa kilomita 53.9.

Alisema sheria za barabarani zikisimamiwa vizuri pia itasaidia barabara kudumu na kutumika kwa muda mrefu.

Alisema baada ya kufanya ukaguzi na kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), wamejiridhisha na ujenzi huo ambao sasa umepunguza usumbufu na gharama kubwa kwa wananchi.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa barabara mkoani humo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD), Rogatus Mativila, alisema barabara hiyo inaunganisha Mkoa wa Njombe na nchi jirani za Malawi na Zambia.

Alisema barabara ya Njombe Makete ilijengwa kwa kugawanywa katika sehemu kuu mbili, Njombe-Moronga kilomita 53.9 na Moronga-Makete kilomita 53.9 ambazo zimekamilika na zinafanyakazi vizuri.

Mhandisi Mativila alisema barabara hiyo ilijengwa na makandarasi wawili tofauti imegharimu Sh. bilioni 243 na kukamilika Agosti 31, 2022.

Awali, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe, Deo Sanga, alisema fedha zilizoletwa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa barabara zimesaidia barabara kufunguka, kutokana na wakazi wa Makete hadi Mbeya kutolazimika kuzunguka kwenda Njombe.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 500 kwa ajili ya kukata mlima Kimelembe uliopo wilayani Ludewa kwa ajili ya kuanza mradi wa Liganga na Mchuchuma.

Kamati hiyo pia imekagua ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe na kukagua mradi wa uboreshaji wa mtandao wa maji mjini humo.

# Kesi ya anayedaiwa kuwaua bibi, babu yaanza kusikilizwa ushahidi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza imeanza kusikiliza kesi ya mauaji inayomkabili mkazi wa Kahama, Emmanuel Kulwa (36) anayeshtakiwa kwa kuwaua Donadi Kasika (70) na Kalekwa Kazembe (60) kwa kuwacharanga mapanga na kufariki dunia papo hapo kisha kuwatumbukiza kwenye shimo la choo.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Jaji Mfawidhi wa mahakama hiyo, Ntemi Kilekamajenga.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Monika Matwe, ulidai una mashahidi wawili wa kuwasikiliza.

Jaji alikubaliana na ombi hilo na kumuuliza Wakili wa kujitegemea Raulent Bugoti anayemtetea mshtakiwa kama yuko tayari, wakili alijibu yupo tayari kusikiliza mashahidi wawili wa upande wa Jamhuri.

Shahidi wa kwanza upande wa Jamhuri ambaye ni mtoto wa marehemu hao, Elizabert Mashauri (45) akiongozwa na Wakil i wa Serikali Monika Matwe, alidai Machi 29, 2020 majira ya saa nane mchana akiwa nyumbani kwake, watu watatu walifika na kumwambia katika shule ya msingi wameona nguo za mama yake zikiwa na damu, ambazo ni shuka, gauni na kanga.

Mashauri alidai baada ya kupata taarifa hizo aliongozana na watu hao hadi sehemu ya zilipokuwa nguo na kukuta watu wengi wamekusanyika akiwamo mshtakiwa Kulwa ambaye ni mtoto wa dada yake aliyekuwa akiishi na wazazi wake.

Alidai kuwa alimuuliza Kulwa nguo za mama yake zimefikaje shuleni wakati yeye ndiye anaishi na wazazi wake na alimjibu kwamba hajui.

Baada ya majibu hayo alimuomba ufunguo wa nyumba ya wazazi wake na mshtakiwa aliutoa mfukoni na kumkabidhi.

Alidai alipofika nyumbani kwa wazazi wake alifungua mlango na kukuta panga na shoka yakiwa na damu na chini karibu na mlango kukiwa na damu, alipofuatilia damu hizo hadi kwenye shimo la choo aliwakuta mama yake mzazi na baba yake wemetupwa humo na wameshafariki dunia.

Alidai baada ya kuona miili ya wazazi wake alianguka na kuzimia na alipozinduka aliambiwa na wananchi aende kumona mama yake kwa mara ya mwisho na alimuona mshtakiwa amekamatwa akiwa ndani ya gari la polisi.

Alidai Machi 30, 2020 alipata taarifa kuwa Kulwa aliamua kuwaua bibi na babu yake ili achukuwe mashamba na ayauze ili akanunue pikipiki.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili wa kujitegemea Laurent Bugoti, ulimuuliza shahidi taarifa za mshtakiwa kuuza mashamba ili anunue pikipiki alizipata wakati gani.

Shahidi alijibu kuwa baada ya msiba wa wazazi wake.

Upande wa Jamhuri, kupitia Wakili wa Serikali Monika Matwa, ulimwambia Jaji Mfawidhi Kilekamajenga kuwa kuna shahidi wa pili na yuko tayari kumsikiliza.

Jaji alikubaliana na ombi hilo na kumuuliza Wakili wa kujitegemea Bugoti ambaye anamtetea mshtakiwa kama yupo tayari kumsikiliza shahidi wa pili upande wa Jamhuri na alijibu yuko tayari.

Shahidi wa pili wa upande wa Jamhuri Dk. Josefu Francis (59), akiongozwa na Wakili wa Serikali alidai yeye ni daktari msaidizi wa Hospitali ya Mkoa wa Geita anakumbuka Machi 29, mwaka 2020 majira ya saa nane mchana aliambiwa na mkuu wake wa kazi aende Kijiji cha Bukori kufanya uchunguzi wa miili miwili na alipofika alimkuta askari polisi na wananchi wakiwa wameshaitoa kwenye shimo la choo.

Alidai marehemu Kasika alikuwa na majeraha matatu sehemu za kichwani upande wa kulia na jeraha kubwa lilikuwa katikati ya kichwa ambalo lilikata mshipa wa damu na kusababisha kumwaga damu nyingi.

Pia, Kazembe alikuwa na majeraha usoni na chini ya sikio upande wa kulia, jeraha chini ya sikio lilikata mshipa wa damu na kusababisha damu nyingi kumwagika.

Alitaja sababu ya vifo ni ubongo kukosa hewa. Baada ya kumaliza uchunguzi wa miili ya marehemu hao alijaza fomu mbili za uchunguzi na kumkabidhi askari polisi na kuondoka kurudi kazini Geita.

Jaji aliahirisha kesi hiyo hadi kesho kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maofisa wanaokaidi maagizo ya Bunge wachukuliwe hatua

**KAMATI** za kudumu za Bunge zimekuwa zikiibua mambo mbalimbali katika taasisi za kisekta za serikali kulingana na majukumu yao. Miongoni mwa mambo yanayoibuliwa ni madudu yanayofanywa katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ufujaji wa fedha za umma na miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

Kutokana na kuwapo kwa madudu hayo, kamati hizo zimekuwa zikiandaa taarifa za utekelezaji wa kazi na kuziwasilisha Bungeni na kufanya Bunge kutoa maagizo mbalimbali ikiwamo kujibu hoja kuhusu mambo yaliyobainishwa. Maagizo hayo huwa maazimio ya bunge ambayo hutoa nafasi kwa wizara pamoja na taasisi zilizo chini yao kutoa majibu au kutekeleza yale yanayowahusu.

Juzi, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), ilipokea majibu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambayo yalionekana si ya kuridhisha kutokana na maazimio 12, hivyo kutoa wiki tatu kuwasilishwa majibu ya uhalisia. Miongoni mwa maazimio ambayo yamekosa majibu ni hatua zilizochukuliwa dhidi ya halmashauri 155 zilizobainika kushindwa kukusanya marejesho ya Sh. bilioni 47 yanayotokana na mikopo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Kutokana na kutokuridhishwa na majibu hayo ambayo kimsingi yalitokana na hoja za ukaguzi za mwaka 2020/21, kamati hiyo kupitia mwenyekiti wake, Halima Mdee, ilisema suala la mikopo katika halmashauri limekuwa 'donda ndugu' kutokana na mambo yanayokwenda kinyume na ilivyokusudiwa. Kuwapo kwa kasoro hizo, Bunge lilielekeza mamlaka za nidhamu kuchukua hatua dhidi ya halmashauri zilizobainika kushindwa kukusanya fedha hizo zilizotolewa kama mikopo kwa makundi husika.

Sambamba na mikopo, kamati hiyo ilibainisha kwamba miradi mbalimbali katika halmashauri ikiwamo vituo vya mabasi na masoko imekuwa hasara kwa mamlaka hizo kwa kuwa fedha zinazopatikana katika maeneo hayo ni kidogo, hivyo kushindwa kuchangia kikamilifu mapato ya ndani. Katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama maji, elimu, afya na barabara, serikali imekuwa ikitoa mabilioni ya shilingi kila mwaka ili kuwaondolea wananchi adha za ukosefu wa huduma katika maeneo yao.

Licha ya kusudi jema la serikali, baadhi ya watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia sekta hizo, wamekuwa wakishirikiana na makandarasi kufanya miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango. Pamoja na hayo, katika baadhi ya halmashauri, fedha hizo zimekuwa zikichepushwa na kwenda kufanya shughuli zingine tofauti na ilivyokusudiwa. Kuhusu mikopo ya halmashaurim ni dhahiri kwamba fedha zinazotolewa kwa makundi hayo, ambazo ni asilimia 10 za mapato ya ndani katika halmashauri, zinalenga kuwakwamua kiuchumi wananchi, kwa kuwataka wale wanaonufaika kuzirejesha ili ziwafikie wengine. Kwa kufanya hivyo, wananchi hao wanaondokana na utegemezi na hali duni kimaisha na matokeo yake kujenga uchumi imara kuanzia ngazi ya mtu mmoja, familia, jamii hadi taifa kwa ujumla. Lakini inapofikia hatua mpango huo unatekelezwa kinyume cha makusudi ya serikali, ikiwamo watendaji kushindwa kusimamia urejeshaji wake, inaonekana wazi kwamba watu hao wanahujumu nia njema ya serikali katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi.

Mbaya zaidi ni pale mamlaka za serikali zinapotoa majibu mepesi kwa maswali magumu juu ya maazimio ya Bunge kuhusu mambo yaliyoibuliwa na kamati za Bunge pamoja na ukaguzi unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Wakati umefika sasa kwa mamlaka za nidhamu kuwawajibisha wale wote wanaohusika na utendaji mbovu katika halmashauri kama vile maofisa maendeleo ya jamii walioshindwa kusimamia urejeshaji wa fedha za mikopo kwa makundi maalum.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wanawake mnaaminika kwa umakini, msichague kazi

**NAKUMBUKA** miaka ya 1980 na hata kabla ya hapo, kulikuwapo mama aliyetushangaza wengi wakati huo, kwa kuendesha basi la Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).

Mwanamke huyo alijizolea umaarufu wakati huo, kwa sababu mbalimbali. Kuu zaidi, haikuwa kawaida kwa wakati huo kumuona mama anayeendesha gari, hata madogo tu ilikuwa adimu.

Katika zama hizo akawa anaendesha basi kubwa la abiria, lilikuwa ni jambo la ajabu na umma ukavutiwa kumuona. Tukiwa wadogo sana, tulipenda kukaa mbele tu ya basi kumuona anavyoendesha, huku akizipangua gia.

Kingine, hakuwa tu dereva hivi hivi, alikuwa na misimamo mikali na hakusita kusimamisha basi na kupambana na yeyote atakayeonekana kujihatarisha kwa kutoa kichwa dirishani, au mkono nje, maarufu kuweka kishoka. Mama huyo alibarikiwa mwili, hata kubeba sura ya umwamba, ukiongeza na kujiamini kwake.

Naambiwa, baadaye aliacha kazi na kujiunga na kampuni za usafirishaji mikoani, akiendesha malori ya tela safari za nje ya nchi.

Pamoja na wengi kumshangaa, baadhi ya wanawake wakavutiwa, hata akawabadilisha mitazamo, baadhi ya wanaume na kinamama, kuhusu dhana kazi za kike na kiume.

Taratibu tukaanza kumuona mwanamke akiendesha magari ya Umoja wa Mataifa (UN). Kama vile haitoshi, kuna mwanamama naye akawa dereva wa kampuni moja ya mabasi kwenda mikoani mwanzoni mwa miaka ya 2000 .

Yalikuwa mapinduzi makubwa. Tulikofika leo, hakuna anayeshituka akimuona mwanamke anaendesha gari. Wako wengi mno. Kwenye magari 10 unayoyaona, unaweza kukuta manne yanaendeshwa na kinamama.

Halafu sasa, ukiona yanaendeshwa nao ujue ni ya kwao, tofauti na wanaume, wengi ni madereva, wanaomiliki ni wachache.

Hili limenijia, baada ya kumsikia Mtendaji wa kampuni za Bravo Logistics na Agricom Africa, Angelina Ngalula, akiwaambia wanawake kuacha kuchagua kazi, badala yake wachangamkie fursa ambazo wana uwezo nazo kuzifanya.

Maana yake wasiweke kando zinazoitwa za kiume, muhimu ni kama wanamudu kuzifanya, hapo asisahau kutaja dereva wa magari makubwa, hasa malori. "Ili wanawake waonyeshe kuwa wana uwezo, kitu wanachohitaji si nafasi za upendeleo au kubebwa, bali wajengewe uwezo wa kuwezeshwa kimtaji, ikiwemo mikopo," alisema Ngalula ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Nikupongeze kwanza Ngalula kwa kuliona hilo na kuwahimiza kinamama kuchangamkia fursa.

Niseme tu, kwa miaka ya hivi karibuni wanawake wameonekana kuamka na kuanza kufanya shughuli au kazi ambazo miaka ya 1970 hadi 1990 mwanzoni, hawakuonekana kuzifanya.

Penye ukweli, lakini unashangaza, kazi nyingi zinazofanywa na wanawake leo, zamani zilionekana za wanaume. Sasa kinamama wanazifanya kwa ufanisi, umakini na uhakika zaidi.

Hata ajali za barabarani, mara nyingi ni za kinababa, wanawake daima wako makini sana na wanafuata zaidi sheria za usalama barabarani. Hata ukikuta ajali inamhusisha mwanamke, basi yeye gari lake litakuwa limegongwa.

Nimekuwa nikishuhudia hata kazi ya utingo na konda wa daladala , zamani ilionekana ya wanaume tu. Leo kinamama vijana, mjini, wameshaanza kuiteka. Wanaifanya kwa ufanisi, wao na abiria wanakuwa wanafurahia huduma zao.

Kwenye mabasi ya umma zamani usiku kuanzia saa saba, au alfajiri ilikuwa si rahisi kumkuta mtoto wa kike, lakini sasa unaweza kukuta basi usiku lina wanawake wengi kuliko wanaume.

Mfano Dar es Salaam, wengime saa hiyo wanaenda Feri kuchukua samaki, wengine kwenye machinjio kupata nyama, ili warejee kuuza supu, wengine kwenye masoko makubwa kuwahi bidhaa za jumla, ili waje kwa rejareja, ili mradi tu 'kazini inaendelea.' wamejichanganya maeneo wakifanya vema.

Hata kwa soka, wanawake nchini sasa wanafanya vema, kiasi hata kwenye timu ya taifa, imefanikiwa sana na kutwaa makombe mengi, ikiwami kushiriki fainali za Kombe la Dunia la Vijana hivi karibuni.

Pamoja na hayo, bado, wapo wanaojifikiria. Niseme, wasonge zaidi kwa kujitokeza, wameshaonekana wakiingia wanafanya vizuri kwa umakini zaidi, kuliko wanaume.

HABARI KITAIFA

# Utafiti waonesha wahitimu kutumia ujuzi katika kujiajiri

**Na Joseph Mwendapole**

UTAFITI uliofanywa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) mwaka 2022 kuhusu fursa za ajira kwa wahitimu, umeonesha kuwa asilimia 79.5 ya wahitimu waliopitia chuoni hapo, wanaweza kutumia ujuzi walioupata katika ajira zao.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na wakuu wa mashirika na taasisi mbalimbali kupata maoni yao kuhusu namna ya kuboresha kozi za chuo hicho.

Alisema utafiti huo ulionyesha kuwa asilimia 59.5 ya wahitimu walikuwa wameajiriwa katika mashirika ya umma na binafsi, wakati asilimia 20 wamejiajiri lakini ni asilimia 20.5 tu ndio bado wanatafuta ajira.

"Hali hii inaonesha kuwa CBE iko kwenye njia sahihi na haitasimama katika maboresho yoyote ndiyo sababu mkutano kama huu ni muhimu kwa wadau kutoa maoni na tunathamini maoni yako tunawaomba wafanyakazi wenu waje katika chuo chetu kwani kuna programu zetu kumi za Shahada za Uzamili ambazo sasa zinaendelea kufanya vizuri katika soko la ajira," alisema.

Alisema CBE kwa miaka mingi, imejikita katika utafiti na ushauri wa kitaalamu ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya biashara na ndiyo maana mwaka 2017 chuo hicho kilikuwa mwenyeji wa kongamano la "Applied Research Conference on Africa (ARCA)" miaka sita iliyopita kwa mafanikio makubwa.

Alisema ARCA ni kongamano kubwa barani Afrika ambalo hushirikisha wataalamu wa juu katika masuala ya maendeleo yanayogusa maisha ya waafrika na kwa miaka mitatu mfululizo chuo kimekuwa kikifanya kwa mafanikio "Kongamano la Maendeleo ya Biashara na Uchumi jijini Dodoma "Business and Economic Development Conference (BEDC).

"Hii huwaleta pamoja wadau na wataalamu mbalimbali kujadili masuala kadhaa yanayohusu ukuaji wa uchumi na maendeleo. Kwa njia hii CBE imeleta mageuzi kwai jamii za Tanzania na Afrika kwa ujumla inatosha kusema Chuo ni zaidi ya kufundisha masomo ya biashara lakini pia kinafanya na kitaendelea kufanya mambo mengi zaidi kwa manufaa ya kijamii ," alisema.

Alisema baada ya takribani miaka 58 ya uwepo wa CBE sasa chuo hicho kinakaribia kuwa na eneo la elimu bora ya biashara na ujuzi kwa mtu yeyote anayetaka kufanikiwa katika biashara ndogo za kati na kubwa nchini Tanzania.

CBE kilikuwa chuo cha kwanza cha elimu ya biashara Tanzania ambacho kilizinduliwa rasmi na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1965 na tangu wakati huo kimeendelea kujikita katika kutoa elimu ya biashara nchini.

"Naomba niwaarifu kuwa CBE imezalisha wataalamu wengi wenye ujuzi hadi sasa na kipindi hiki chuo kimeongeza udahili na kuanzisha kozi zingine, zikiwemo za Utalii ili kuunga mkono juhudi za serikali.

"CBE imeendelea kutoa kozi za elimu ya biashara kwa miaka mingi kwa kiasi kikubwa kutokana na ongezeko la uhitaji na Chuo kuona umuhimu zaidi kutokana na mwitikio wa wananchi kutoka kwa wanafunzi mbalimbali kujaza vyuo vyetu jijini Dar es Salaam tangu mwaka 1965," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Lwoga, CBE inaendelea kudahili wanachuo zaidi katika programu za uzamili katika Kampasi za Dar es Salaam na Dodoma.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation, Asma Mwinyi (kushoto), akikabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vya kuchezea watoto kwa Mkuu wa Kitengo cha Ustawi wa Jamii katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Asha Salum, jijini Dar es Salaam jana kwa lengo la kuwafariji watoto wanaoumwa magonjwa ya moyo wanaotibiwa kwenye taasisi hiyo. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Bigger Heart Zanzibar, Layla Yahya. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Wapiga simu kutaka kuuza figo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, amewaonya baadhi ya watu hususani vijana kupiga simu mara kwa mara hospitalini hapo wakiuliza utaratibu wa kuuza figo ili wapate fedha za kujikimu.

Dk. Chandika alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa maadhimisho ya miaka mitano ya upandikizaji figo yaliyofanyika katika ukumbi wa hospitali hiyo alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema amekuwa akipokea simu kutoka kwa vijana ambao wanamuuliza kama hospitali hiyo inahitaji kununua figo na kwamba wengi wao amekuwa akiwapa elimu kwamba sheria ya nchi hairuhusu kuuza viungo.

"Mimi binafsi nimepokea simu za vijana wanne nilichowaambia kama wana ndugu wana tatizo waje wawasaidie kuwapa figo lakini hapa hatununui wala kuuza figo," alisema Dk. Chandika.

Alisema Hospitali ya Benjamin Mkapa inasimamia sheria za nchi zinavyoelekeza kwa kutoruhusu biashara ya viungo vya binadamu na jamii inapaswa kulielewa hilo.

Hata hivyo, alisema hospitali hiyo itaendelea kuwaelimisha ndugu, jamaa na marafiki ya kuwa wanafanya kazi ya utoaji huduma ya kupandikiza figo na si kuuza figo kama baadhi ya vijana wanavyofikiria.

Akielezea kuhusu wagonjwa ambao wametoa figo zao nakuwapatia wagonjwa ambapo hubakia na moja Dk. Chandika amewatoa wasiwasi kwani kabla ya kuitoa nakupandikizwa wanafanya uchunguzi wa kina nakujiridhisha kwanza ili mtoa figo asipate athari kiafya.

Faraji Shaban, ambaye alipandikizwa figo hospitalini hapo kutokana na matatizo ya kiungo hicho, alisema hivi sasa anaendelea vizuri na anafanya shughuli zake kama kawaida.

Shaban alisema alipatwa na matatizo ya figo yake kushindwa kufanya kazi vizuri kuanzia mwaka 2017 na alifanikiwa kupandikizwa mwaka 2019 iliyotolewa na mwanawe na sasa anaendelea na shughuli zake kama zamani japo alisema gharama ni kubwa kama mtu anajilipia.

"Uwapo wa huduma hii hapa nchini inatusaidia sana gharama ni kubwa, lakini huwezi kulinganisha na nje ya nchi,"alisema Shaban. Hospitali hiyo ya Benjamin Mkapa kuanzia mwaka 2018 hadi 2023 imependikiza figo kwa wagonjwa 33 kati ya hao 22 wamepandikizwa na wataalam wazawa na wote wanaendelea vizuri.

Gharama za upandikizaji figo katika hospitali hiyo ni Sh. milioni 35 na hiyo ni kuanzia maandalizi mpaka upandikizaji unakamilika.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Bunge lataka SUA kuwezeshwa kifedha

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo imeitaka serikali kuendelea kukipatia fedha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kiendelee kufanya utafiti na ugunduzi mkubwa na kujiimarisha zaidi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hayo juzi wakati kamati hiyo ilipotembelea chuo hicho kwa ajili ya kukagua miradi ambayo serikali imetoa fedha na inatekelezwa sambamba na kujionea mafunzo kwa vitendo.

Alisema kamati imejionea namna chuo hicho kilivyojipanga kuhakikisha wanafunzi wanaopita hapo wanatoka na stadi za maisha kuanzia katika ngazi mbalimbali, zikiwamo za kilimo, udaktari wa wanyama na ufugaji wa samaki na kwamba wengi hawazungumzi kwenda kutafuta ajira bali kujiajiri.

Pia alitoa wito kwa wanafunzi wa shule nchini kuwa na msukumo wa kusoma sayansi sababu ndipo ilipo dira ya maendeleo ya nchi na pia kwa maisha yao ya baadaye huku wakizingatia kujiunga na SUA ambayo imejipanga katika kutoa utaalamu wa umahiri.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, alisema tayari serikali imeshaona umuhimu wa maeneo hayo hasa kwenye utafiti.

Kwa sasa kuna mradi wa zaidi ya dola za Kimarekani milioni 425 sawa na zaidi Sh. bilioni 972 za Kitanzania zinazopelekwa kwenye vyuo vikuu nchini.

Alisema fedha hizo zitapitia mradi wa mawasiliano kiuchumi kwa elimu ya juu (HEAT) na kupelekwa kwenye maeneo mtambuka ya sayansi, teknolojia na ubunifu pamoja na maeneo ya kilimo.

Naibu Waziri alitoa wito kwa chuo hicho kuhakikisha kinasimamia fedha vizuri ambazo ni fungu kwa ajili ya SUA kwa ajili ya kuendeleza chuo cha Katavi kwa kujenga baadhi ya majengo sambamba na baadhi ya fedha kutumika Morogoro, ikiwamo kusomesha wataalamu wakiwamo wenye digrii mbalimbali kwa kuziongeza.

Kipanga alisema fedha hizo zaidi zinapelekwa katika eneo la utafiti na ubunifu na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuliona eneo la utafiti kwamba ndilo litakalowaondoa wanafunzi katika nafasi za chini na kuwapeleka katika nafasi za juu zaidi.

Awali, Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema chuo hicho kina watumishi 1,389 na wanafunzi 16,379 wanaosomea shahada mbalimbali.

Alisema sambamba na kutoa elimu mbalimbali lakini pia SUA ndio mahiri kwa nchi za kusini mwa Afrika kwa masuala ya upandaji na utunzaji misitu na wengine wanakuja kujifunza.

Mbunge Mwakilishi wa Vyuo Vikuu, Dk. Thea Ntara, alishauri elimu na mafunzo mazuri yakiwamo ya ufugaji samaki na kilimo katika kituo atamizi isambazwe kwenye matawi mengine ya SUA likiwamo la Tunduru, ili wananchi hasa vijana wajifunze na kuwa na nafasi ya kujiajiri.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, akizungumza na wananchi pamoja viongozi mbalimbali kuhusu umuhimu wa elimu ya kilimo bora kwa wananchi wote wilayani humo, alipofanya ziara ya kijiji kwa kijiji juzi. **PICHA: STEVEN WILLLIAM**

# Serikali yataka wadau nishati kujadili mazingira

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imewataka wadau wa nishati safi ya kupikia (LPG) kutoka mataifa mbalimbali waliokutana jijini Dar es Salaam, wajadili masuala ya mazingira na afya na matumizi ya LPG kama mbadala wa kupikia.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, aliyasema hayo juzi Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya LPG Afrika Mashariki - Tanzania 2023.

Maonyesho hayo yamehudhuriwa na washiriki zaidi ya 800 kutoka mataifa tofauti pamoja na kampuni 50 zinazoonyesha bidhaa za LPG.

Mkurugenzi wa LPG Expo, Catherine Ho akisoma hotuba ya Mhandisi Mramba, alisema tukio hilo ni jukwaa kuu la kuleta hadhi ya sekta ya LPG na ajenda ya nishati safi ya kupikia nchini.

"Tuna wajumbe wa kigeni hivyo, tutakuwa na nafasi ya kujifunza uzoefu kutoka nchi nyingine kwenye uwanja wa biashara ya LPG na kutambua tunavyoweza kunakili mbinu bora na kujifunza kuhusu mazoea mabaya kufanya mambo ili tuweze kuboresha," alisema.

Alisema mambo makuu ya Sera ya Taifa ya Nishati ya 2015 ni pamoja na kuendeleza rasilimali za nishati za ndani ambazo ni chaguzi za gharama nafuu na kukuza bei ya nishati ya kiuchumi.

Pia alisema kuboresha utegemezi wa nishati na usalama na kuongeza ufanisi wa nishati; kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi; kupunguza uharibifu wa misitu na kuendeleza rasilimali watu.

"Tunaamini wakati wa mijadala katika hafla hii ya siku mbili tutapata fursa ya kujadili masuala ya mazingira na afya wakati wa kujadili sekta ya upishi ambayo katika nchi yetu ina sifa kubwa ya nishati asilia kama vile mkaa na kuni," alisema.

Aidha, aliwaeleza washiriki hao kuwa manufaa ya kutumia LPG kama nishati mbadala ya kupikia, gharama, uhamasishaji, masuala ya usalama kwa matumizi ya nyumbani ni miongoni mwa maeneo ambayo wanahitaji kupata uzoefu.

Alisema ajenda ya kongamano hilo inahusu sekta mbalimbali, kutoka kwa mahitaji ya LPG, mtazamo wa ugavi na bei.

Pia alisema inahusu LPG kama chanzo cha nishati safi na nafuu; fursa ya uwekezaji katika biashara hiyo; kukuza usalama, ubora na viwango; Ukuzaji wa Usalama na Mazingira Kiafya (HSE) ili kukuza Maendeleo Endelevu ya LPG.

Pia alisema inahusu wajibu wa viongozi wanawake katika kukuza nishati safi ya kupikia nchini Tanzania.

Catherine alisema wameandaa kongamano hilo ili kuchochea mjadala wa nishati safi na kukuza matumizi ya gesi katika matumizi mbalimbali kwa maendeleo endelevu.

# Muswada mabadiliko sheria ya reli waiva

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imesema inakusudia kufanya mabadiliko ya Sheria ya Reli kwenye Bunge la Bajeti litakaloanza Aprili, mwaka huu, ili kuruhusu sekta binafsi kutoa huduma na kuleta ushindani katika sekta hiyo.

Moja ya sababu ya kurusu wawekezaji wazawa na kutoka nje ni kurudisha gharama kubwa za ujenzi wa mradi wa reli, na kwamba mpaka sasa serikali ishatoa Sh. trilioni 23.5 kwa mradi mzima kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Tabora hadi Kigoma.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema hayo jana wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Miundombinu kutembelea na kukagua mradi wa Reli ya Kisasa ya Umeme (SGR) kipande cha Morogoro hadi Makutupora.

"Serikali imekuja na mpango mbadala wa kubadilisha Sheria ya Reli kuwe na watu binafsi ambao watatumia miundombinu hii ya reli na kwa mara ya kwanza muswada ushasomwa bungeni katika Bunge lililopita la mwezi wa pili," alisema Mwakibete na kuongeza:

"Tunategemea bunge la mwezi wa Machi, Aprili hadi Mwezi wa sita tupitishe sheria itakayoruhusu hata sekta binafsi waweze kuwekeza katika reli yetu, kwa maana ya kuwa na 'return investment', kwani thamani ya mradi ni Sh. trilioni 23 ili iweze kurudi ni kuruhusu wawekezaji binafsi kuleta vichwa vyao vya treni, watakaoleta mabehewa yao ili iwe kama mfumo wa barabara unavyotumika," alisema.

Aliongeza kuwa hatua hiyo itasaidia kupunguza gharama kwa TRC na kuifanya reli kuwa na tija na kuongeza ufanisi na ushindani kwa kuruhusu sheria hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, Seleman Kakoso, alisema kamati ipo tayari kusapoti bungeni mpango huo katika mabadiliko yatakayofanyika katika sekta hiyo.

"Napenda kuwahakikishia serikali, tupo tayari kushirikiana nao kufanya mabadiliko haya makubwa ili kuhakikisha ushiriki kamili wa sekta binafsi, ili kupunguza gharama na kurudisha gharama ya uwekezaji mkubwa uliofanyika chini ya Rais Samia Suluhu," alisema.

Pia Kakoso aliutaka uongozi wa TRC kumsimamia mkandarasi, ili kuhakiksha miradi yote inakamilika kwa wakati kwa mujibu wa mkataba kwa muda uliopangwa na kutomwongezea muda ndani ya mkataba.

Kwa mujibu wa Kakoso, kumekuwa na ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi ya SGR kwa sababu zisizokuwa na ushawishi hali inayopoteza muda mwingi wa utekelezaji na serikali kushindwa kutimiza malengo yake.

"Watu wanataka kuona miradi inakamilika kwa wakati na waweze kufanya shughuli zao za kimaendeleo, ili kwetu liwe somo na kusitokee kucheleweshwaji wa miradi mingine na kuichonganisha serikali na wananchi.

Pia ameutaka uongozi wa TRC kuhakikisha mwekezaji anaacha ujuzi kwa vijana na kwenye miradi kuwapo wazawa ambao watapata mafunzo ya kuendesha miradi hiyo.



# Meneja mgodi mbaroni madai kuhamasisha maandamano

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

JESHI la Polisi mkoani Manyara, linamshikilia Meneja wa Mgodi wa Gem & Rock Venture, Joel Mollel, kwa tuhuma ya kuongoza wachimbaji wadogo kuvamia mgodi wa madini ya tanzanite ulioko eneo la Kitalu C katika Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro.

Mgodi wa Kitalu C unaochimbwa kwa ubia kati ya serikali na mwekezaji mzawa, Onesmo Mbise, unadaiwa kuvamiwa Machi 12, mwaka huu majira ya mchana na kundi hilo, wakiwa na silaha za jadi.

Katika vurugu hizo, kundi la wachimbaji hao wanadaiwa kuwajeruhi zaidi ya wafanyakazi 10 wa kampuni hiyo ambao hali zao zinadaiwa kuwa ni mbaya, kwa sasa wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, iliyoko mkoani Kilimanjaro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, alisema kuwa polisi walifanikiwa kumkamata Mollel kwa madai ya kwamba ndiye alikuwa kiongozi mkuu wa uvamizi huo. Kamanda Katabanzi alisema kwa sasa Mollel anahojiwa katika Kituo Kikuu cha Polisi Mirerani. Alisema mbali ya Mollel Jeshi la Polisi linawashikilia baadhi ya watu wengine ambao ni wafanyakazi wa Kampuni ya Gem & Rock Venture, kampuni inayomiliki mgodi wa tanzanite uliko kitalu B mpakani wa mgodi wa Kitalu C unaochimbwa na kampuni ya Franone unaomilikiwa na Mbise.

Kampuni ya Gem & Rock Venture unaomiliki mgodi wa tanzanite ulioko kitalu B unamilikiwa na mfanyabiashara maarufu jijini Arusha, Sammy Mollel ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (TAMIDA).

Hata hivyo, Kamanda Katabanzi alisema kama utaratibu wa upelelezi na mahojiano ukikamilika huenda wakafikishwa mahakamani kujibu mashtaka. Kamanda Katabanzi alisema: "Tumemkamata Saitoti (Mollel), Meneja wa Kampuni ya Gem & Rock Venture, kwa kuwa anatuhumiwa kuwa alikuwa kiongozi wa kuongoza genge la wavamizi katika mgodi wa serikali na mbia mwenza,"alisema Kamanda Katabazi.



Naibu Waziri wa Madini, Dk. Stephen Kiruswa (wa tatu kulia), akizungumza na wafanyakazi wa Barrick, alipotembelea maonyesho katika mkutano wa jukwaa la pili la utekelezaji wa ushirikishwaji Watanzania katika sekta ya madini jijini Arusha jana. Kulia ni Meneja wa Barrick nchini, Dk. Melkiory Ngido. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Waziri aonya matukio ya ubadhirifu mali za umma

**Na Hamida Kamchalla,** KOROGWE

WANANCHI wa Kata ya Mswaha, Wilaya ya Korogwe, wametakiwa kuacha vitendo vya ubadhirifu wa mali za umma, badala yake waweke ulinzi kwenye miundombinu ambayo imepelekwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umeme vijijini.

Rai hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Steven Byabato, akiwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) walipofanya ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini wilayani humo.

Byabato ambaye ni Mbunge wa Bukoba Mjini, alisema kuna baadhi ya maeneo serikali imepeleka miundombinu lakini wako baadhi ya wananchi wamefanya hujuma.

"Tumeletewa miundombinu hii tuilinde kwa kuwa maeneo mengine zilipelekwa nguzo na nyaya zikaibiwa, makandarasi wanahofia vitu kulala kwenye maeneo ya mradi, kwa hiyo tuvilinde kabla havijasimikwa ili viendelee kutunufaisha," alisema. Akifungua kikao mbele ya wananchi wa eneo hilo, Diwani wa Kata ya Mswaha, Hassan Mdigo, alisema suala la umeme katika kata hiyo, limekuwa kilio cha muda mrefu, hivyo serikali imefanya jambo ambalo wananchi mwanzo hawakuamini kama nishati hiyo ingeweza kuwaka kwenye maeneo yao.

Alisema kata hiyo ina vijiji sita vyenye vitongoji ambavyo ni vikubwa lakini havikuweza kuingizwa katika mpango wa awali wa umeme, hivyo ameiomba serikali kufanya jitihada za kuwapatia nishati hiyo ili kila mwanakijiji aweze kunufaika na maendeleo yanayoletwa na serikali yao.

"Umeme ni kero kubwa ya muda mrefu, tunaishukuru sana kamati kwa kushirikiana na mbunge wetu, kutuwashia umeme katika Kijiji cha Mswaha Darajani kwa sasa na sisi tunajiona ni Watanzania kwa kuwa tumekumbukwa kwa kupatiwa umeme.

"Mswaha tulikuwa tunahitaji umeme kwa kuwa tumezindua kijiji kimoja na baada ya hapa tutakwenda Kijiji cha Tabora na baadaye vijiji vingine, naiomba kamati hii kuangalia mpango wa kuingiza umeme kwenye vitongoji vikubwa kabla ya mwaka 2025," alisema Mdigo.

Meneja wa Usimamizi wa Miradi (REA), Romanus Lwena, alisema mkandarasi anatekeleza miradi hiyo katika wilaya tatu za Mkoa wa Tanga ambazo ni Korogwe, Pangani na Mkinga inayogharimu Sh. bilioni 25 na miradi Korogwe ikigharimu Sh. bilioni 12.

# RC atoa angalizo matukio ya moto Mlima Kilimanjaro

**Na Mary Mosha** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro imesema endapo matukio ya moto yakiendelea kutokea katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA) baada ya miaka mitano mlima huo hautakuwapo.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliyasema hayo baada ya kuendelea kuzuka kwa matukio ya moto, ujangili, uvamizi na shughuli za kibinadamu katika hifadhi hiyo.

Babu aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa mdahalo ambao ni sehemu ya kumbukumbu ya maadhimisho ya miaka 50 ya KINAPA.

"Kwa sasa hali ni mbaya, matukio ya moto, ujangili yameshamiri, tumeanza kupata hadi matatizo ya maji katika mji wetu, tukifanya mchezo hiyo ilikuwa ni miaka 50 nyuma ambayo tumeifikisha, lakini tusipojizatiti hakutakuwa na Mlima Kilimanjaro tena baada ya miaka mitano ijayo,"alisema Babu.


Hata hivyo, aliitaka KINAPA kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaofanya ujangili na vitendo ambavyo vinaharibu uoto wa asili katika mlima huo.

"Watu wanaofanya tabia za ovyo kwenye hifadhi wachukuliwe hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine, mimi ndiye Mkuu wa Mkoa huu, sintamvumilia mtu yeyote atakayebainika kufanya shughuli za kibinadamu zitakakazohatarisha uoto wa asili katika Mlima Kilimanjaro,"alisema Babu.

Naibu Kamshna wa Uhifadhi TANAPA, Steria Ndaga, alisema wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo na ujangili, migogoro ya mipaka pamoja na uchomaji moto.

"Matatizo haya ni pamoja na ujangili wa wanyama pori, kuendelea na shughuli za kibinadamu katika msitu kama vile ukataji wa nyasi, uokotaji kuni pamoja na migogoro ya mipaka,"alisema Ndaga.

Baadhi ya wadau na waongoza watalii katika Mlima Kilimanjaro, Damian Mwombo, aliiomba serikali kuangalia upya magari ya nyaya kwa kuwa bado kuna matatizo mengi ikiwamo kupoteza ajira kwa vijana.





## Ahukumiwa kwenda jela miaka 30 kwa kumbaka mtoto

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKAZI wa Kariakoo, Kata ya Kitete mkoani Tabora, Seleman Sengo (39), amehukumiwa kwenda jela miaka 30 kwa kosa la kumbaka mtoto wa miaka 11 (jina limehifadhiwa).

Mtoto huyo ambaye ni wa kambo alimlaghai kuwa atamnunulia sambusa baada ya kutekeleza adhima yake.

Akitoa hukumu hiyo juzi, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Tabora, Singwa Mzige, alisema kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Mei 5, mwaka 2022 majira ya jioni katika eneo la Kariakoo.

Hakimu Mzige alisema mtuhumiwa alimdanganya mtoto huyo na kumpeleka nyumbani kwake na kutekeleza unyama huo.

Alisema mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo kufuatia Sheria ya Makosa ya Ubakaji Kifungu cha 130 Kifungu Kidogo Namba 1 na 2 Kipengele 'e' na Kifungu cha 131 cha Kanuni ya Adhabu ya Mwaka 2019.

Inaelezwa kuwa mtoto huyo aliondoka nyumbani na kwenda kwa rafiki zake kwa ajili ya kuangalia TV ambako mshtakiwa akamfuata na kumwambia waondoke wote akamnunulie sambusa nyumbani.

ilielezwa kuwa baada ya kufika nyumbani mshtakiwa akamwambia mtoto avue nguo kisha kuanza kumbaka.

Awali akitoa ushahidi mahakamani hapo, mama mzazi wa mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alisema alipoona mtoto wake amechelewa kurudi nyumbani akaamua kumfuata kwa rafiki zake.

Alieleza kuwa alipofika kwa rafiki yake hakumkuta ndipo akaamua kwenda kwa mshtakiwa huyo (mume wake wa zamani) na alipofika alimkuta mtoto wake anatoka ndani kwa kukimbia.

Alisema baada ya kumuuliza mtoto wake akasema baba yake wa kambo amembaka kwa kumdanganya kuwa atamnunulia sambusa, hakujua kama atamfanyi kitendo hicho.

Akiwa mahakamani hapo, mshtakiwa katika utetezi wake alikana kufanya tukio hilo.Hata hivyo, mahakama hiyo ilimhukumu kwenda jela miaka 30 kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Wakili wa Serikali, Joseph Mwambalulu, aliiambia mahakama hiyo kuwa kitendo kilichofanywa na mshtakiwa huyo ni kinyume cha sheria, hivyo hukumu iliyotolewa iko sahihi kulingana na kosa alilolifanya.



Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Shishinulu, Kata ya Isaka, wilayani Kahama mkoani Shinyanga jana, wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira, kukagua miradi ya maji ya Kagongwa-Isaka na Tinde-Shelui. Kushoto ni Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jackson Kiswaga. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Bunge laagiza miradi ya TASAF kuboreshwa, inufaishe jamii

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, imeshauri miradi ambayo imekuwa ikiibuliwa na walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia mpango wa kunusu kaya maskini iboreshwe na iwe na viwango ili kuleta manufaa katika jamii.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara, ufugaji, kilimo, biashara na shughuli za ufundi wa aina mbalimbali ambazo zikiboreshwa zitawanufaisha wao binafsi pamoja na jamii kwa ujumla.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Florent Kyombo, alibainisha hayo juzi wakati kamati hiyo ilipotembelea mradi wa walengwa wa TASAF, Mtaa wa Mwadui, Kata ya Ngokolo. Alisema kuibuliwa kwa mradi wa barabara hiyo na miundombinu mingine ni hatua nzuri kwa wanufaika hao, kumshauri Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) kuzipitia barabara hizo ili kuziboresha ziwe za kiwango kuliko zilivyo hivi sasa.

Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, aliagiza kuwa miradi hiyo ya TASAF ambayo inaibuliwa na walengwa hasa ya barabara washirikiane na TARURA ili kuimarisha ubora wake.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema wataendelea kuisimamia miradi yote ambayo inatekelezwa na walengwa wa TASAF ili iwe na ubora zaidi pamoja na matumizi sahihi ya fedha zitolewazo kwa walengwa hao.

Alibainisha kuwa katika Mkoa wa Shinyanga kuna miradi ya TASAF 598 na fedha zilizoletwa ni Sh. bilioni 51.14 kwa ajili ya kufanikisha miradi hiyo.

Habiba Shango ni miongoni mwa wanufaika wa TASAF, alipongeza serikali kwa kuendelea kutoa fedha na kutekeleza miradi ya maendeleo, ambayo imekuwa ikiwaingizia kipato na kuendesha maisha yao.

# Madiwani wamwomba mwindaji kuwaua wanyama hatarishi

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Sengerema limeridhia mwindaji wa wanyamapori hatari wilayani humo, Paulo Pasian, kuwawinda wanyama ambao wamekuwa tishio kwa kuvamia, kujeruhi na kuua wananchi katika wilaya hiyo.

Hivi karibuni wilayani Sengerema yameripotiwa matukio mbalimbali ya wananchi kushambuliwa na wanyama kama vile fisi, mamba na mbwa ambao wamekuwa wakiongezeka kila siku na kusababisha hofu kwa wananchi.

Hatua hiyo imesababisha baraza hilo kuridhia kumruhusu mwindaji, Paulo Posian kuanza kuwawinda na kuwadhibiti wanyama hatarishi wakati mamlaka husika zikiendelea kutafuta suluhisho la muda mrefu.

Hatua hiyo ilifikiwa katika Baraza la Madiwani kwenye kikao cha robo ya pili ya mwaka 2022/2023 na kuwasilisha kilio chao kwa Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri hiyo juu ya kuweka mwindaji atakayedhibiti matukio ya mara kwa mara yanayosababishwa na wanyama hao wakali.

Sospiter Busumabu ni Diwani wa Kata ya Tabaruka alisema katika kata yake kumekuwa na ongezeko la mbwa pamoja na fisi ambao wamekuwa wakizagaa mida ya saa kumi na mbili jioni na kusababisha hofu kwa wakazi wa maeneo hayo huku wengine wakiwashambulia watoto.

Diwani wa Kata ya Chifufu, Robarth Madaha, alisema kwenye kata yake kuna mamba ambao wamekuwa wakiwadhuru wananchi wanaoenda kuchota mji pamoja na wavuvi na kusababisha vifo kwa wananchi, hivyo kushauri kuwekwa mikakati madhubuti ya kudhibiti wanyama hao.

Akitoa taarifa ya hali ya uhifadhi, Kaimu Ofisa wa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira, Benadetha Fransisco, alisema idara hiyo inatambua uwepo wa wanyama hao hatari na kusema kuwa tayari wamepeleka pendekezo wizarani kwa ajili ya kupata ufumbuzi juu ya hao wanyama.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Sengerema, Yanga Makaga, alisema kwa kipindi hiki ambacho bado idara hiyo inatafuta suluhisho la kudumu dhidi ya wanyama hao anatakiwa kuwapo mwindaji wa wanyama hao ili kuondoa hofu kwa wananchi.


Ukurasa 12

Machimbo mapya ya graphite kupaisha uchumi Ruangwa, pia zawadi ajira 1600


Ukurasa 13

Wanaolawiti na kunajisi watoto, adhabu iliyopo leo bado haitoshi


BUFE
IJUMAA MACHI 17, 2023
Nipashe


Ukurasa 14

**MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA**
**Mbunifu Rose Urio : Ahsante mama kukaribisha vazi 'Batiki Mshumaa'**

MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA

# Dk. Mpango na Waziri Mwigulu walivyotoa ushuhuda kikaoni Doha makubwa ya nchini




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, walipokuwa kikaoni, jijini Doha Qatar, siku chache zilizopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**Na Jenifer Gilla, aliyekuwa,**

**Doha, Qatar**

NI keshokutwa Dk. Samia Suluhu Hassan, anatimiza miaka miwili ya urais. Ikiangaliwa, je katimiza yapi na ana mwelekeo upi katika kuongoza Watanzania?

Nyuma yake ana safu kamili ya kuchapa kazi, msaidizi mkuu wa kwanza, ni Makamu wa Rais Dk.Philip Mpango, ambaye hadi wiki moja iliyopita, alikuwa jijini Doha, nchini Quatar, akimwakilisha rais katika Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi zinaoendelea za Kipato cha Chini (UNLDC5).

Hiyo ilikuwa kati ya tarehe nne na tisa mwezi huu, nchi 46 duniani zilikutana kujadili watavyokomboa nchi zao na janga hilo, mjadala kuzama katika Mpango wa Utendaji wa Doha (DPoA).

Kimsingi, unaowekewa mkazo mambo matano, ikiwamo elimu ya chuo kikuu kutolewa kwa mtandao, ili kukuza ubora wake na kujengewa uwezo wa kuboresha usalama wa chakula na ushirikiano na nchi zinazoendelea katika kuleta maendeleo.

Mengine, ni kuwapo kituo cha msaada wa kuongeza uwezo wa kustahimili athari za mabadiliko ya hali ya hewa, kupitia kurekebisha na kuboresha mfumo wa tahadhari kama vile kujengwa madaraja, kuta za kuzuia maji ya bahari na kuvamia makazi na kuboresha miundombinu ya barabara.

Ni mpango unaotarajiwa utazisaidia nchi kukabiliana na vikwazo vinavyorudisha nyuma maendeleo yao, ikiwamo kukosa kutoa elimu bora na usaidizi wa kuhitimu katika kundi la nchi zenye kipato cha chini, kukabiliana na usalama wa chakula na mfumuko wa bei za vyakula na msaada katika uwekezaji.

**MIKAKATI YA TANZANIA**

Tanzania nayo iliwasilisha mkutanoni hapo, mikakati yake kuboresha teknolojia, ili itumike kukuza uchumi wa nchi na taifa kujikwamua kutoka katika umasikini.

Kimsingi, unalenga kuzishinikiza nchi zilizoendelea zitoe msaada wa hali na mali, hata kujiletea teknolojia ya kisasa itakayotumika kukuza uchumi kwa njia ya ushirikiano.

Akiwasilisha mada mkutanoni, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema Tanzania inakaribisha ushirikiano wa kuhamisha teknolojia ili kujiongezea uwezo wa nyenzo za maeneo mbalimbali, ikiwamo upatikanaji wa chanjo.

Anasema ni teknolojia anayoitegemea kuiunganisha Tanzania na watu bilioni tano duniani kote mtandaoni, huku watu bilioni mbili wanaotumia biashara ya mtandaoni wakifikiwa na asilimia 60 ya Pato la Taifa, linalopitia njia za kidigitali.

Hivyo, anaeleza nchi imedhamiria kupunguza umasikini na kukuza uchumi ambao mpaka mwaka jana umerekodiwa kukua kwa asilimia tano kwa mwaka,

baada ya kusuasua hadi asilimia 4.8 mwaka 2020, ilhali kabla ilikuwa asilimia 6.7 kabla ya janga la Uviko -19.

Anataja maeneo wanayochangia kukua uchumi, inajumuisha nidhamu, sera rafiki ya fedha, mageuzi endelevu ya kitaasisi na udhibiti wake, pamoja na kuchukua hatua kukabili misukosuko ya kiuchumi, kwa kushirikisha wazawa.

Mengine anaorodhesha ni kugatua mfumo wa afya, ushirikiano wa kimkakati, utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Usambazaji wa Chanjo ya COVID-19 na Mpango wa Majibu ya Kijamii, ikiendana na

majadiliano ya kusamehewa au kusimamishwa kwa madeni.

Kwa kipekee, Waziri Dk. Nchemba, anataja kampeni ya filamu 'Royal Tour' imekuwa na nafasi yake katika mapinduzi ya sekta utalii.

Anasema Mpango wa Utendaji wa Doha (DpoA), unaonyesha matumaini kwa nchi kuondakana na umasikini,unaosababishwa na changamoto kama za mikopo mikubwa, mfumuko wa bei za chakula duniani na kuongezeka gharama kwenye miradi ya maendeleo.

Akifafanua hoja hizo, Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, anasema Tanzania imeweka kipaumbele kuwekeza katika maeneo muhimu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo nishati ya jua na upepo, usimamizi bora wa taka na teknolojia rafiki kwa mazingira.

Dk. Mpango anasema hadi sasa nchi inashuhudia athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo matukio makubwa kama ya ukame na mafuriko, mvua zisizotabirika, kupanda kina cha bahari na baadhi ya visiwa kuzama, vyote vikisababisha uhaba wa chakula, migogoro ya kijamii na kupanda gharama za maisha, hata kudororesha uchumi

Anaongeza kuwa, Tanzania inakadiriwa kuwa na hasara ya kiuchumi kufika Dola za Marekani milioni 33.7 katika kipindi

**INAENDELEA UK.14**

UCHUMI

# Machimbo mapya ya graphite kupaisha uchumi Ruangwa, pia zawadi ajira 1600

## • Wenyeji 59, kila mmoja atwaa nyumba mpya

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYANI Ruangwa kuna mradi mpya unaohusu kuzalisha madini aina ya grafaiti au 'graphite', ambayo faida yake ya awali ni ujio wa jumla ya ajira za kudumu na za muda, jumla yake 1600 kabla na wakati wa uzalishaji.

Hayo ni madini yanayotumika kutengeneza penseli, huku kielektroniki inaelezwa inasaidia kupitisha joto na umeme, mfano kwenye betri na paneli ya sola, hivyo inachangia kuunda nyenzo za kielektroniki.

Mkurugenzi Mkazi wa kampuni Magnis Energy Tanzania, Peter Tsegas, anaiambia Nipashe kwamba ushirikiano wao na kampuni tanzu, Uranex, zote za Australia zimeshakamilisha kulipa fidia wananchi 1,140, watakaoupisha mradi huo, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Mkurugenzi Peter, ambaye pia ni Mwendeshaji Mkuu wa mradi, anasema kampuni kwa sasa inamiliki eneo la kilomita za mraba 30 zenye kiasi kikubwa cha madini bora, baada ya utafiti uliokuwapo tangu mwaka 2013.

Kwa mujibu wa bosi huyo wa mradi ulioko Nachu, inakadiriwa kuzalisha kwa miaka 16, lakini tafiti zaidi zinaonyesha uwezekano kufika miaka 40, kila mwaka kuzalishwa tani 230,000 za grafaiti.



Baadhi ya nyumba zilizojengwa na wawekezaji wa mradi madini ya grafaiti, ikiwa ni fidia ya makazi yao wilayani Ruangwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**FIDIA ZILIVYOENDA**

Anafafanua kwamba wananchi watakaolipwa fidia ni walioathiriwa na mradi kabla mshauri huru alipotumika kuhakiki madai, kwa kuzingatia viwango vya kimataifa (IFCPS) kama vilivyoainishwa na Benki ya Dunia (WB).

Peter anaeleza, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilishirikishwa kuhakikisha haki ya fidia ya ardhi na hatua ya kwanza walitakiwa kuhamisha makazi yao.

"Jumla ya nyumba 59 zimejengwa ndani ya viwanja 56 ambavyo vilinunuliwa na Uranex, zilikabidhiwa kwa ajili ya kuwahamishia wananchi, kutokana na kwamba eneo lilikuwa pori wenye makazi ya kudumu walikuwa wachache," anabainisha.

Vilevile anasema, eneo la mradi lilikuwa na nyumba 59, akidokeza hatua inayofuata ni kujengea wakazi huduma za kijamii kama za afya na soko.

**MANUFAA YA MRADI**

Kwenye manufaa ya kiuchumi, mkuu huyo wa mradi anasema utakuwa na manufaa kutokana na kwamba, ni malighafi muhimu yanayogusa utengenezaji bidhaa kama betri za magari na umeme.

"Dunia ya sasa iko kwenye magari ya umeme katika kuhakikisha matumizi ya teknolojia safi ambayo haiharibu mazingira," anasisitiza.

Pia, anafafanua utekelezaji wa mradi huo una sura ya manufaa kiuchumi, kwa kushuka chini kwa jamii zinazozunguka mradi na nchi kwa ujumla, kupitia mahitaji ya bidhaa na huduma zinazotolewa na kampuni za ki-Tanzania na wazalishaji wengine wa Ruangwa.

Mkurugenzi huyo anasema, ni takriban miaka 10 tangu mradi huo wa madini uanze na kuna maendeleo kwa wakazi tangu zama za utafiti, mara baada ya kupatikana leseni.

"Sasa tuko kwenye hatua ya ujenzi wa awali ambao umeshaanza," anasema.

**HALI YA AJIRA**

Mkurugenzi Peter anafafanua, anasema kipaumbele kilichopo ni kwa wananchi, kupata mafunzo ya kilimo, ufundi vyuma, magari, lengo ni kuwainua kiuchumi.

Anasema, umeelekezwa kuboresha huduma za jamii kwa maendeleo endelevu ya mradi na wanauona ustawi wa wilaya hiyo, akitoa mfano mradi ulipoanza walilazimika kuagiza bidhaa kama nyama, kuku, matunda na mboga kutoka Dar es Salaam, lakini sasa zinazalishwa na wananchi, jambo wanalojivunia.

**ATHARI MAZINGIRA**

Mkurugenzi huyo anasema, wamejipanga kuhakikisha wanatumia nishati safi, ili kupunguza uchafuzi wa mazingira na wako katika mazungumzo na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika hatua pana zaidi.

Anataja eneo la kufungwa bomba lenye urefu kilomita 90, kusafirisha gesi asilia kutoka Mingoyo kwa ajili ya uzalishaji na kupunguza matumizi ya nishati chafu kama mafuta ya dizeli.

Anasema, pia magari yao yanatumia injini ya gesi asilia kupunguza gesi ukaa kwenye mazingira yao, akinena kuwa uchakataji madini ya grafaiti hauhitaji kemikali zenye sumu kama zilivyo aina nyingine za madini.

"Tujitahidi kadri ya uwezo wetu kupunguza kusambaa kwa vumbi katika eneo la mradi tuna kifungu cha kufunga uzalishaji madini, ambacho kinatutaka kurejesha mazingira ya eneo la mradi katika hali yake ya awali, mara shughuli za mradi zitakapofikia mwisho wake," anasema.

**KUISAIDIA JAMII**

Peter anasema mradi haujaanza rasmi, ila ukianza wana matarajio wenyeji watanufaika sana na huduma za elimu na afya kwa watoto wao, ikijumuisha kukarabatiwa shule na zahanati.

Pia anasema, hadi sasa wameshagawa vitabu vya sayansi kwa shule za sekondari na kushiriki kwenye shughuli mbalimbali, ikiwamo maadhimisho ya Siku ya Wanawake wilayani humo.

Ni aina ya mjumuiko na ushiriki wakutumia bajeti Sh.milioni 250 kwa shughuli za kijamii, lengo ni kuhakikisha wenyeji wanufaika na shule tajwa.

**CHANGAMOTO IKOJE?**

Mkurugenzi huyo anasema, changamoto zilizopo ni upatikanaji mtaji wa kuendeleza stahiki kutokana na sababu mbalimbali, huku miradi ya bidhaa za grafaiti duniani, zikiwa kwenye ushindani mkubwa wa soko.

Anataja shida nyingine ni ubovu wa miundombinu, ambayo utatuzi wake uko kwenye kushirikiana na serikali kufikia maboresho yake.

MAGEUZI MAKAMBAKO, NJOMBE NA IRINGA

# Neema Mfuko UTT unavyosafiri na mapya ya teknolojia

**Na Elizabeth Zaya**

HADI sasa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Duniani inakuwa kwa kasi. Vivyo hivyo, sekta ya biashara na hasa ndogo nchini, nayo inapanuka kwa kasi, hata kuchangia kwa kiasi kikubwa uchumi, wahusika nao wakizama kwenye TEHAMA.

Hapo ndipo, Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Utafiti la nchini Canada (IDRC), limeungana nayo, kwa kufadhili mradi mkubwa wa utafiti kati ya mwaka 2008 na 2010 katika miji ya Makambako na Njombe na Mkoa wa Iringa, lengo ni kutathmini matokeo ya TEHAMA katika maendeleo ya biashara ndogo.

Ni mradi wa majaribio unaohusisha makundi mawili ya wafanyabiashara wenye uwiano sawa, kwani uwekezaji wa kutumia TEHAMA umetajwa kuwamo katika orodha yanayotajwa kuongeza kasi ya uchumi kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo, pia mtu mmoja mmoja.

Inajumuisha nyenzo simu katika mabadiliko hayo, ikiwa na faida nyingi kiuchumi, ikiwamo katika kuendesha miamala yako ya kifedha.

Vilevile, zinafahamika kusaidia malipo mbalimbali, kama sokoni, dukani, huduma za afya, za maji, umeme na kodi za nyumba, viwanja na bima.

Pia, katika suala la uwekezaji, simu nayo ina nafasi yake, ikiwa ni daraja la kusaidia kuchukua na kuweka fedha kwenye akaunti za benki.

**UTT&TEKNOLIJIA FEDHA**

Kupitia Mfuko wa Umoja (UTT AMIS) unaotajwa kuwa wa wazi, nao unaelezwa kusaidia kuepusha upotevu wa fedha ndogo, hususani kwenye miamala ya kila mara, kama ilivyo katika simu, hapo ikimsaidia mfanyabishara kuendesha shughuli zake.

Ni mfuko unatoa fursa mtu kuwekeza kiwango kisichozidi asilimia 50 ya fedha zake kwenye hisa zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa Dar es Salaam na asilimia 50 zinaachwa kwenye masoko mengine ya fedha na mitaji yenye sifa tofauti.

Sera ya uwekezaji kwa upande mmoja, ni mpango madhubuti uliowekwa na mfuko huo ili kutawanya rasilimali zake na kwa upande mwingine, ni mpango mkakati wa kinga endapo eneo moja la uwekezaji likifanya vibaya.

Aidha, uwekezaji kwenye hisa katika mfuko huo hufanywa kwa kiwango cha chini, ikilinganishwa na eneo lenye mapato ya kudumu.

UTT ni mfuko wa kwanza kuanzishwa na umekuwa sokoni tangu mwaka 2005, ukitoa faida kati ya asilimia 10 mpaka 20.

Hadi sasa mfuko unamuwezesha mfanyabiashara kuchukua fedha, akawekeza kwenye akaunti yake ya uwekezaji UTT AMIS kupitia simu, hata ikasaidia kumkatia bima ya afya.

Faida nyinginezo inatajwa kupitia uwekezaji katika mfuko huo, ni kuokoa muda, haraka ya miamala na usalama wake na kuongeza mzunguko wa fedha kwenye uchumi.

Ni mfuko ambao mtu au mfanyabiashara, anaweza kuunganisha simu yake na ya benki kumrahisishia kufanya miamala kwa haraka, bila ya kupoteza fedha kwa makato, kama ilivyo katika uwekezaji mwingine tofauti nao.

Tafiti zinaonyesha watu hutumia hadi asilimia 30 ya fedha zake, kwa kutokuwa makini na teknolojia hizo zinazotumika kufanya miamala mbalimbali ya kifedha, na fedha hupotea zaidi kadri kiwango cha fedha kinachofanyiwa muamala.

Uwekezaji wa pamoja kupitia UTT AMIS, hutoa fursa ya majibu kwa magumu hayo, ambayo mtu anawekeza fedha kidogo, ambayo kwa namna mbalimbali hutumika vibaya au hupotea.

Hadi sasa mfumo huo uko katika hatua ya maendeleo, ukitoa fursa ya watu kuungana na kuchanga katika mfuko mmoja, kisha wanaziwekeza katika mfuko wa UTT AMIS, huwekezwa ukizingatia waraka wa makubaliano, usalama, uwazi na taratibu zote kwa malengo ya kuzipa pesa thamani zaidi.


Uwekezaji unaanza na shilingi 10,000, inayowekwa kupitia simu ya mkononi au benki, hadi kufika kwenye akaunti binafsi ya UTT AMIS.

Inashauriwa, jambo la kuzingatia ni kuwekezwa katika mfuko ikiangaliwa fedha binafsi tu anazitenga kutoka kipato chake, Mwekezaji kwenye mfuko huo wa umoja anaweza kuuza vipande vyake muda wowote.

Inaelezwa kwamba, fedha anaipata mhusika ndani ya siku 10 za kazi, tangu alipowasilisha maombi, pasipo kuwapo kizuizi au gharama za kuuza vipande hivyo vya mfuko akiwa na unafuu mkubwa wa kodi.

Mara zote, tathmini ya thamani halisi ya Mfuko, hukokotolewa kila siku ya kazi na kutangazwa, huku usalama wa fedha za mwekezaji ukitajwa kuwa mkubwa, kwa sababu mfuko unasimamiwa na taasisi ya serikali inayoaminika, ikitoa faida shindani, ukwasi na usalama kwa fedha za mwekezaji.

TAFAKURI YA MLALAHOI




# Wanaolawiti na kunajisi watoto, adhabu iliyopo leo bado haitoshi



NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
(kulangwasos@gmail.com)

ZAMANI familia na kaya mbalimbali zilishi kwa kupendana, kuaminiana, kuelewana na kushirikiana karibu katika kila jambo. Mtoto wa familia hii alikuwa mtoto wa familia nyingine.

Kama mtoto alikwenda nyumba jirani akakuta wanakula, alikaribishwa na kukaa na kula na wenzake, walicheza pamoja na hata usiku waliweza kulala pamoja salama.

Yote hayo yalifanyika bila majirani kuhitilafiana wala kuvunjiana imani, kwani walikuwa sawa na ndugu waliozaliwa pamoja. Watu walialikana katika shughuli mbalimbali bila hiyana.

Mabadiliko ya tabia za watu yakasababisha mambo mengi yaliyoleta mgawanyiko na tofauti za kiimani na hivyo kujengeana chuki kati ya mtu na mtu, kati ya familia na familia au kaya na kaya.

Leo hii ni nadra sana kukuta mtoto wa jirani anakula kwa jirani na hiyo ni kutokana na ama kukatazwa na wazazi au walezi wake, kula kwa jirani au jirani kumnyima tu, akidhani anakuja kudowea kutokana na ukata wa kwao.

Wazo la mtoto kudowea huko nyuma halikuwapo, kwa sababu chakula kilikuwapo cha kutosha na hivyo mtoto kula kusingepunguza lolote. Ndiyo sababu pia mtu kama alikuja kwako, akakuta umeanika muhogo au kiazi, alichukua na kutafuna pasipo kuomba.

Leo hii thubutu! Nenda nyumbani kwa mtu ukute ameanika kiazi au muhogo na ujichukulie utafune bila kuomba, kama hutakuta kesi kwa mjumbe wa mtaa na kutakiwa kulipa fidia! Imani imekwisha!

Chuki na ukosefu wa imani vilipoanza kuibuka baina ya majirani, ikajikita pia ndani ya familia yenyewe. Zamani watoto walilala chumba au kitanda kimoja na wageni au ndugu na kutoka salama.

Leo hii ukimwacha mwanao na mgeni na kumlaza naye chumba kimoja, kwa asilimia kubwa anaweza asitoke salama. Matukio ya watoto kunajisiwa au kulawitiwa yamekuwa mengi nchini kwa sasa.

Hivi sasa bora mgeni wa kiume, ukamchukulie chumba kwenye nyumba ya kulala wageni kuliko kumlaza na wanao chumba kimoja. Hakuna heshima tena hakuna woga wala kujali, watoto wanaonewa watoto wanatendwa.

Wazazi, walezi na viongozi wa serikali wamebaki kulalama na kupiga kelele majukwaani na kwenye vyombo vya habari wakikemea tabia hizo chafu zilizoota mizizi katika jamii.

Katika majumba ya ibada ambako tulidhani ndiko liliko kimbilio la wanyonge, hivi sasa nako hakufai, viongozi wa majumba hayo nao wanatajwa kujihusisha na matukio hayo machafu.

Shuleni,vyuoni na kokote kunakotolewa mafunzo ya dini, mambo kama hayo yamefika. Afadhali yafanywe kwa watu wazima wanaojitambua, lakini kwa watoto ni mbaya na kwa kweli ni kufuru hata kwa Mwenyezi Mungu.

Wanakamatwa watu wakifanya vitendo hivyo dhidi ya watoto, wanafikishwa mahakamani na kuhukumiwa vifungo vya miaka si chini ya 30 jela na wengine maisha. Lakini, mbona vitendo hivyo havikomi?

Yameanzishwa madawati ya jinsia katika vituo karibu vyote vya Polisi nchini inatolewa elimu kuhusu ubaya na athari za vitendo hivyo, lakini mbona watu hawakomi?

Wanaofungwa wanafungwa, lakini hatimaye nasikia wananufaika na misamaha na kurudi uraiani kuendelea na uchafu huo dhidi ya watoto wetu, malaika wasiojua lolote!

Tutaendelea kulea uovu huu hadi lini? Ni lini watu wenye akili mbovu kama hawawatakoma? Yasemekana matendo haya mengi huhusishwa na imani za kishirikina. Je, wanaoshawishi mambo haya hawapo kweli?Tuwafanyeje ili kuokoa maisha ya wanetu?

Kulawiti, kubaka au kunajisi mtoto mdogo ni kumuua kimaisha. Kama tunakubaliana hilo, kwanini wahusika wasiuawe? Tunajua ipo sheria ya wakosaji kunyongwa sambamba na wauaji, waasi na wazinzi katika baadhi ya imani.

Tunajua pia kuwa ipo sheria ya kimataifa ya haki za binadamu inayotetea binadamu kuwa na haki ya kuishi. Je, kama yeye hataki wenzake waishi, kwanini yeye aishi? Tuchukulie matatizo ya ulawiti na unajisi kama matatizo sawa na mauaji.

Tukiendelea kukumbatia sheria hizi za haki za binadamu na kuacha binadamu wafanye matendo ambayo hata wanyama hawayafanyi, basi tujue watoto wetu tunawatelekeza mikononi mwa mafirauni.

UCHUMI

MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA

# Mbunifu Rose Urio, kinamama : Ahsante mama kukaribisha vazi 'Batiki Mshumaa'

## • Waona njia 'itawatoa' kwa hadhi, kiuchumi

**Na Pilly Kigome**

KADRI siku zinavyoenda, ndivyo mjadala wa kuwapo vazi la taifa unavyopamba moto, kinamama hasa ndio wamelikamata.

Hapo kunatajwa vazi liitwalo 'Batiki Mshumaa'. Hakika lilipendezesha na kupamba Siku ya Wanawake Duniani, hivi karibuni. Cha mvuto ni ushuhuda, kinamama wengi wakiwa wamejikuta wakikosa vazi hilo, ingawa walihamasika, sababu kuu ni wauza vifaa na malighafi kumaliza bidhaa zao.

Ni zao la ukubwa wa mwitikio wake, katika kupamba sikukuu hizo. Mbali na vazi hilo kupendezesha sikukuu za kitaifa, tayari linachukua sura ya kuwa rasmi, kutokana na ukweli wa mwitikio hadi namna linavyopendezesha sikukuu za kiserikali, kukawapo juhudi kubwa za kutetea ukuaji wa soko hilo.



Kinamama wakiwa katika vazi lao la batiki.**PICHA:MTANDAO.**

**KINACHOFANYIKA**

Mkurugenzi Mtendaji wa asasi Royal Progress Centre, Rose Urio, ndiye amejikita mstari wa mbele katika dai hilo la vazi na soko, ambalo linainua maradufu juhudi za matumizi ya batiki ndani na nje ya nchi.

Hadi sasa inatajwa, wameshafanikisha kwa kiasi kikubwa kutokana na uhalisia, tayari serikali imeshalikubali vazi hilo katika sikukuu za kiserikali nchini na kwa mwaka huu, sikuuu hiyo ya wanawake ndio imefungua mlango katika vazi hilo.

Rose anaiambia Nipashe kwamba, wamepambania hilo kwa kiasi kikubwa kukua kwa vazi hilo na sasa wanaishukuru serikali iliyopo madarakani, imeitikia wito, vazi batiki livaliwe kitaifa katika sikukuu hizo.

Sasa anatoa wito kwa Rais Samia, awe balozi namba moja katika vazi la batiki, alisimaie na kulitumia katika safari zake za nje ya nchi na kubeba kiasi kadhaa, anazotoa zawadi.

Anatoa mtazamo wake, kwamba mkuu wa nchi atakapofikia hatua hiyo, itakuwa na maana kubwa inayoleta tija kwa soko la batiki ya Tanzania duniani, ikiwamo kuwainua wanawake wazalishaji kiuchumi.

Pia, anafafanua kwamba, binafsi hakuona haja ya kuzalisha nguo za batiki na kuzipeleka katika soko la dunia, pale alipoenda nchini Marekani mwaka 2021.

Anafafanua kuwa, hatma hiyo inatokana na pale akagundua batiki nyingi alizoziona madukani, nembo zake zinaonyesha kutoka nchi jirani na za Tanzania zilikuwa chache.

Rai yake ni kwamba, hadi sasa umefika wakati Watanzania wachangamkie fursa, kwani walitaka kuanza na soko la Agoa, lakini wamegundua pia, soko kubwa pia liko ndani ya nchi.

**MWANZO WA MAFANIKIO**

Kwa mujibu wa Rose, hadi kufika Julai 8, mwaka jana, walishazindua Siku ya Batiki katika Viwanja vya Maonyesho vya Sababasa, Dar es Salaam, lengo ni kuitangaza batiki katika soko la dunia kwamba, mradi huo upo Tanzania Bara na Visiwani.

Hapo anawasilisha shukurani zake kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuwapatia ridhaa ya kuvalisha batiki hilo la kitaifa.

Kwa mara ya kwanza katika sikukuu hiyo ya wanawake, kumetokea mafuriko ya wateja wa soko hilo, kwa kuwa waliweza kuzalisha zaidi ya nguo milioni nne na bado hazikutosha mahitaji.

"Matarajio yetu makubwa kila mwezi tuwe tunazalisha batiki zisizopungua milioni nne, ziende kwenye masoko ya kimkakati Afrika Mashariki, lenye watu milioni 283.7, soko la SADC lenye watu 379.67, soko huru la Afrika na lenye watu bilioni 1.3, soko la Agoa" alisema.

Kuelekea Miaka Miwili ya Rais Dk. Samia, Ruswe anasema wameshapata mafanikio makubwa yanayovunja rekodi, kupata upenyo wa kuvaliwa vazi hilo, huku masoko mengine yakianza kufunguka.

Anasema, mafanikio hayo yana sura kwamba batiki ilianza Tanzania tangu miaka ya 1960, lakini ushuhuda wa sasa umeweka rekodi.

Rose anaeleza hatua wanazochukua katika soko hilo la batiki, ni kwamba wameshafanya mawasilinao na wazalishaji mavazi ya kiubunifu kutoka nchi za Marekani, Uturuki na Vetenam, kuangalia namna ya kupenyeza soko lao huko, kwa kuwa maonyesho ya mavazi hufanya vizuri sana duniani kibiashara.

Rose anaiomba serikali na sekta binafsi, ziwekeze kwa kuwajengea wanawake uwezo wa kutayarisha batiki, ikiwamo kuweka mfumo mzuri wa kupunguza madalali sokoni, ili kuwawezesha wanawake wapate kipato stahiki kinachowaletea tija.

Pia, anasema serikali inapaswa kuwawezesha na kuwaridhia watumie maeneo ya viwanda yasiyotumika sasa, ili kuleta tija katika ubora wa batiki kwa kuwa soko la batiki Tanzania, bado liko chini, kutokana na changamoto ya kutumia majiko ya kuni na mkaa.

Mama huyo anasema, pale ikiridhia kutumika maeneo hayo yanayoombwa, kutawezesha kuletwa tija na batiki itatoka katika ubora stahiki, kwa kuwa watazalisha batiki kwa nishati safi, pia majiko sahihi akitaja ni LPG.

Hapo ana ufafanuzi kwamba kutumia nishati safi kutaleta tija katika soko la dunia kuliko batiki ya sasa inayopikwa kwa majiko ya kuni na mkaa.

**MZALISHAJI MSHIRIKI**

Anna Harold, ni mzalishaji batiki kutoka soko la batiki Mchikichini, Dar es Salaam, aliyepata nafasi ya kuzalisha batiki katika sherehe hizo zilizopita, anasema alifanikiwa kuandaa pisi 1900.

Anasema, mwaka huu kumekuwapo mafuriko ya wateja katika soko hilo, kwamba haijawahi kutokea tangu waanze, akiunga mkono ushuhuda wa awali.

Mama huyo anasema, imewezesha kuzalisha ajira nyingi za muda, kupitia sikukuu hizo kwa kuwa wanawake waliweza kujipatia kipato jumla shilingi 200 katika kusuuza na kuanika kila vazi , ikiwa ni sehemu ya maandalizi.

Anna anaiomba serikali kupitia vyuo vya kati vya ufundi, kuanzisha masomo ya ufundi ikiwamo na upishi wa batiki, kwa kuwa soko kuu la Afrika Mashariki lina idadi kubwa ya watu, kwa hiyo ili kuendeleza soko hilo ni busara kukawepo mfumo bora wa kuleta tija, pia kuwapo wazalishaji wapya,badala ya kuendelea kutegemea waliopo sasa.

**UONGOZI MKOA DAR**

Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Rehema Madenge, anasema mwaka huu serikali inatambua mchango wa wanawake wajasiriamali na imeelekeza vazi batiki litatumika katika sherehe za kiserikali, ili kuwainua kiuchumi wanawake nchini.

Anasema, kutokana na kaulimbiu ya maadhimisho ya siku hiyo ya wanawake kitaifa 'Ubunifu na mabadiliko ya teknolojia ni chachu ya kuleta usawa wa kijinsia', hapo ndipo dhamira kuleta mabadiliko teknolojia jumuishi, serikali inatambua wanawake wajasiriamali wanachangia pato la taifa.

Katika maadhimisho hayo mgeni rasmi katika sherehe hizo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala na akawataka wanawake kutokukatishwa tamaa na baadhi ya wanasiasa wanaobeza kuwa vikoba na biashara ni upuuzi.

# DK. MPANGO NA WAZIRI MWIGULU WALIVYOTOA USHUHUDA KIKAONI DOHA MAKUBWA YA NCHINI

**INATOKA UK.11**

cha miaka 10 iliyopita, kutokana na mafuriko.

Makamu wa Rais anasema, serikali inachukua hatua, zikiwamo kuchimba mabwawa ya maji, kuhamasisha nishati safi ya kupikia, kupanda miti kila mkoa, kujenga kingo ufukweni mwa bahari kudhibiti mmomonyoko wa udongo, kuandaa mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na Mpango Kabambe wa Mazingira wa mwaka 2022 hadi 2032.

Anasema pamoja ya kuwa katika kundi la nchi masikini zenye kipato cha chini, uchumi wa Tanzania unaendelea kukua licha ya kuptiwa na janga la UVIKO-19 na vita vya Ukraine na Russia, ikitumia mikakati wa kikanda, kiserikali na kimataifa na kuongeza ufadhili wa kiuchumi wa masharti nafuu inayoisaidia kupiga hatua za kimaendeleo.

"Tanzania imepiga hatua kubwa tangu mkutano wa Nne wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinaoendelea za Kipato cha Chini (LDC4, uliofanyika miaka 11 iliyopita. Uchumi wetu unasalia kuwa thabiti wenye mwelekeo mzuri…," anatamka Dk. Mpango, ambaye kitaaluma, ni mchumi.





## Simbachawene atoa maagizo watumishi Ofisi ya Waziri Mkuu

**Na Renatha Msungu** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, amewataka watumishi wa ofisi hiyo kutumia rasilimali zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kufanya kazi kwa ufanisi yenye kuleta matokeo chanya kwa taifa.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi hiyo, chenye lengo la kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23.

Simbachawene alisema Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu sehemu ya kazi kwa sababu ni kiunganishi kati ya menejimenti na watumishi, hivyo serikali inazingatia suala la wizara na taasisi zake kuwa na mabaraza ya wafanyakazi.

"Serikali inazingatia sana suala la wizara na taasisi zake kuwa na mabaraza ya wafanyakazi kwani yanaanzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri serikali katika ngazi za idara,"alisema Simbachawene.

Hata hivyo alisema kuwa mabaraza yana majukumu ya kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi, ikiwamo kutoa ushauri kuhusu kujenga hali bora za kazi, maslahi ya wafanyakazi na kusimamia haki na ustawi kazini.

Simbachawene alifafanua zaidi ya kuwa wajibu wa mabaraza haya kama vyombo vya ushauri na usimamizi ni kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao.

Hata hivyo aliishauri menejimenti kupitia baraza hilo kuwa na utaratibu mzuri wa kuwapongeza wafanyakazi wanaotekeleza majukumu yao kwa uweledi ili kuzidi kuwapa moyo wa kuboresha utendaji wao.

Alisema pia kuna watumishi wasomi na wenye wasifu mkubwa lakini wanashindwa kuuonyesha kutokana na mazingira kutokuwa rafiki na kusema baraza linapaswa kuyaangalia hayo ili watumishi wafanye kazi kwa bidii na kuleta matokeo chanya kwa jamii.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, aliwapongeza watumishi wa ofisi hiyo kutokana na kutekeleza majukumu yao kikamilifu ikiwamo kusimamia shughuli za serikali kwa kujituma kama taratibu za kazi zinavyoelekeza.

# RC aagiza wenye nyumba waliokaidi kupanda miti kukamatwa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka viongozi wa ngazi ya kata, vijiji, mitaa na vitongoji kufanya operesheni ya ukaguzi na kuzishtaki kaya ambazo zimeshindwa kupanda miti kama alivyotoa agizo.

Senyamule alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na viongozi na wananchi wa kata na mitaa ya Chang'ombe wakati wa upandaji miti, lililofanyika katika Shule ya Msingi Chang'ombe mkoani Dodoma.

Alisema Serikali ya Mkoa wa Dodoma ilishaagiza kila kaya kupanda miti mitano, hivyo viongozi hao wazisake kaya ambazo zimekaidi kutekeleza agizo hilo la serikali.

Alibainisha agizo hilo la upandaji miti kwa kila kaya ni la nchi nzima na siyo kwa Dodoma peke yake na kuwataka viongozi wasimamie suala hilo na watakaobainika wachukuliwe hatua za kisheria na kushtakiwa.

"Nyinyi viongozi wa kata, vijiji, mitaa na vitongoji hakikisheni kila nyumba mnapita kuangalia kama miti hiyo mitano imepandwa na kwa wale watakaowakuta kaya zao hazina miti wachukuliwe hatua za kisheria, maana hili ni agizo la serikali na lazima litekelezwe,"alisema.

Aidha, aliwataka wazazi na walimu kushirikiana katika kukomesha suala la utoro kwa wanafunzi shuleni, kwa kuwa bado ni tatizo na wasipofanya hivyo wanatengeneza kundi baya la vijana ambao wamekosa elimu.

Awali, akisoma risala ya upandaji miti, Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira Wanawake na Samia Dodoma, Bhoke Mkami, alisema miti 250 imepandwa kwenye eneo hilo la shule ikiwamo 200 ya matunda na 50 ya kivuli. Aliziomba jamii zinazozunguka maeneo inayopandwa miti kuwa walinzi kwa wale wanaoharibu na kuing'oa na kusababisha serikali na wadau wa mazingira kuwakwamisha kufikia malengo yake ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.


Mkami alisema bado kuna tatizo la baadhi ya watu ambao wamekuwa wakiharibu na kuchunga mifugo kwenye maeneo ambayo tayari miti imepandwa.

Alieleza kuwa miti mingi inayopandwa imekuwa ikikosa uangalizi wake hali ambayo imekuwa ikileta hasara kwa wanaharakati na wadau wa mazingira wanaoitikia agizo la serikali ambayo inakuwa mstari wa mbele katika upandaji miti.

"Niwaombe wakazi wezangu ambao tupo karibu na miti hii tunayopanda kwenye maeneo yetu tuwe walinzi kwa wale wanaing'oa na wale wanaochungia mifugo yao ili tusilikwamishe zoezi hili la Dodoma kuifanya kuwa ya kijani," alisema.

Meneja Miradi wa Taasisi ya Helvetas Swiss Inter cooperation, Africanus Chalamila, alisema kuwa wataendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha wadau na wananchi wanaelimishwa katika kutambua umuhimu wa kuwapo kwa miti.

Alisema bado kuna umuhimu wa kuwaelimisha watu ili kutambua miti inayopandwa inatakiwa kulindwa na kutunzwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki, akibonyeza kitufe kuzindua rasmi mfumo wa kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS), baada ya kufungua mkutano wa pili wa Baraza la Wafanyakazi la Tume hiyo kwa mwaka 2022/23 jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, ambaye ni Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Paulina Mkwama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu kidato cha nne wapewa siku 21 kubadilisha masomo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetoa siku 21 kwa wahitimu wa kidato cha nne mwaka 2022 kufanya mabadiliko ya machaguo ya masomo, ili ufanyike uchaguzi watakaojiunga na kidato cha tano na vyuo vya kati.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu Ofisi hiyo, Dk. Charles Msonde, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu wanafunzi waliohitimu kidato cha nne mwaka 2022 ambao wanatarajiwa Julai mwaka huu kujiunga na kidato cha tano.

Alisema wanafunzi 456,975 walifaulu mtihani wa kidato cha nne mwaka 2022 na uchambuzi ulibainisha wanafunzi 192,348 walifaulu kwa madaraja ya juu.

Dk. Msonde alisema wanafunzi hao waliofaulu kwa madaraja ya juu wanaweza kudahiliwa kujiunga na kidato cha tano au vyuo vya kati kwa fani mbalimbali.

"Ofisi ya TAMISEMI ina wajibu wa kuchagua wanafunzi hao waliofaulu kwa kuwapangia kwenye shule na vyuo, na hufanyika baada ya wanafunzi kujaza machaguo yao kupitia fomu ya selform, tumewapa fursa ya kufanya marekebisho ya machaguo yao ili wafanye machaguo sahihi,"alisema.

Msonde alisema kuanzia Machi 14 hadi Aprili 6, mwaka huu wanafunzi hao wanapaswa kutumia fursa hiyo.

"Watumie muda huu uliowekwa, hakutakuwa na muda wa aina yeyote baada ya kupita muda huu uliowekwa, mabadiliko yafanyike kadri itakavyowapendeza na mfumo upo wazi kwa sasa na mabadiliko yazingatie ufaulu wa masomo yao,"alisema.

Dk. Msonde alisema uchaguzi wa tahasusi unafanyika na mfumo kwa ushindani kulingana na ufaulu wa mwanafunzi husika.





# FCC, EWURA, REA, NEMC waagizwa kupitia upya mikataba ya umeme

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, ameitaka Tume ya Ushindani Tanzania (FCC), Mamlaka ya Huduma za Nishati na Maji, (EWURA) Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na Baraza la Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC) kupitia upya mikataba ya wadau wanaosambaza umeme katika maeneo ambayo mkongo wa taifa haujifika.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua kongamano la maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Haki za Mtumiaji Duniani ambayo kitaifa yalifanyika mkoani hapo.

Kigahe alisema lengo la taasisi hizo kufanya hivyo ni kukabiliana na vitendo vya uharibifu wa mazingira pamoja na kudhibiti gharama kubwa ya nishati hiyo.

Alisema ni muhimu mikataba ya wadau wanaosambaza nishati ya umeme mbadala vijijini kuangaliwa upya ili iendane na sera na taratibu zinazomlinda mtumiaji, ikiwamo kupata nishati safi ambayo itasaidia kukabiliana na uharibifu wa mazingira, lakini kuweza kumudu gharama za nishati hiyo.

Aliongeza kuwa kwa kufanya hivyo itasaidia wananchi hususani waishio vijijini na kwa gharama nafuu ukilinganisha na ilivyo sasa ambapo bei ya nishati ni ghali.

"Nataka FCC kwa kushirikiana na mamlaka zote zinazohusika na nishati kupitia mikataba iliyotolewa na watoa huduma za nishati mbadala katika maeneo ambayo mkongo wa taifa bado hujafika, kama haiwakandamizi wananchi sambamba na kuangalia gharama za nishati hiyo kama ni rafiki kulingana na hali halisi ya maisha Watanzania,"alisema Kigahe.

Aliongeza kuwa serikali imepiga hatua katika ukuzaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati nchini, kwamba takwimu zinaonesha kuwa juhudi za kisera, kisheria na kimkakati zimesaidia kuanzisha EWURA, REA, REF na kuongezeka kwa watoa huduma wa bidhaa za petroli na nishati jadidifu nchini.

Mwenyekiti wa FCC, Aggrey Mlimuka, alisema mchakato umeanza wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Kumlinda Mtumiaji ya mwaka 2003.

Alisema sheria hiyo ni ya muda mrefu na haijafanyiwa maboresho hivyo ni wakati sasa wa kuboresha sheria hiyo ili kuendana na mahitaji ya watumiaji kwa sasa.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa FCC, Zaytun Kikula, alisema katika maadhimisho ya tume hiyo yaliyoanza Machi 10, mwaka huu, walitoa elimu kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya( MUST) juu ya umuhimu wa nishati safi kwa mtumiaji ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Aliongeza kuwa elimu hiyo pia ilihusu haki na wajibu wa mtumiaji katika uchumi wa soko sambamba na matumizi ya nishati safi, sambamba na elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari vya Mkoa wa Mbeya.



Ofisa Mkaguzi wa Tume ya Ushindani nchini (FCC), Graciana Gallet, akitoa maelezo ya namna ya kutambua bidhaa bandia na zisizobandia ili kulinda afya ya mtumiaji kwenye kongamano la maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Haki za Mtumiaji Duniani, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Kituo cha kuwafundisha wazazi kulea watoto chaanzishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya WeCare kwa kushirikiana na Hospitali ya Agakhan wamefungua kituo cha maendeleo ya awali ya mtoto kitakachotumika kutoa mafunzo kwa wazazi na walezi wa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto hospitalini hapo.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto jijini hapo, Aquina Mtweve, alipongeza hatua ya taasisi hizo kuamua kuwekeza kwenye ukuaji wa awali wa mtoto hatua aliyosema inalenga kuwezesha kuwa na taifa lililo na rasilimali watu walio na ukuaji timilifu hapo baadaye.

Kuanzishwa kwa kituo hicho ni sehemu ya taasisi binafsi kuunga mkono juhudi za serikali kwenye utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) inayoendelea kutekelezwa katika mikoa 10 nchini ukiwamo Mkoa wa Mbeya.

Mtweve aliwataka wazazi na walezi kutambua kuwa kinachofanywa na serikali na wadau katika kusimamia ukuaji sahihi wa mtoto si maigizo bali kuna faida kubwa, hivyo ni muhimu kwao wakawa tayari kupokea yale wanayofundishwa na wataalamu na kuyafanyia kazi majumbani.

"Tumeona hapa namna ya uchangamshaji watoto kupitia michezo...unaweza ukaona kama ni maigizo au ni mchezo mchezo tu...lakini huu ndiyo msingi muhimu sana wa ukuaji wa mtoto...Wazazi na walezi haya ndiyo tunapaswa kuyafanya majumbani ili kuwajenga watoto kuwa na ukuaji timilifu," alisema Mtweve.

Mratibu huyo wa Afya ya Uzazi na mtoto alishauri taasisi husika na wadau wengine kuona uwezekano wa kufungua vituo vingine kama hivyo kwa kuwa uhitaji ni mkubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasisi ya WeCare, Elizabeth Magunga, alisema walifikia uamuzi wa kufungua kituo hicho baada ya kuona watoto waliokuwa wakiwapokea kwenye kituo chao cha malezi ya awali ya mchana wakiwa na tatizo la ukuaji.

Magunga alisema kupitia kituo hicho sasa wazazi watakaokuwa wakihudhuria kliniki katika Hospitali ya Agakhan na wale watakaofika siku atakazopanga daktari wa watoto hospitalini hapo watapata wasaa wa kukutana na kujifunza kutoka kwa wataalamu.

Aliyataja maeneo makuu matano yatakayozingatiwa kwenye utoaji elimu kwa wazazi kupitia kituo hicho kuwa ni pamoja na afya, lishe bora, malezi yenye mwitikio, ulinzi na usalama pamoja na ujifunzaji wa awali.

Meneja wa Hospitali ya Agakhan Tawi la Mbeya, Michael Mwanisenga, alisema uwapo wa kituo hicho kutaisaidia pia jamii kuondokana na baadhi ya maradhi yanayowakabili watoto yanayotokana na wazazi na walezi kukosa uelewa wa kutosha wa namna ya kuwakinga watoto wao ikiwamo udumavu na utapiamlo. Hivyo aliwakaribisha wadau wengine walio na utayari wa kushirikiana na hospitali hiyo kwenye uwekezaji unaoweza kuisaidia jamii akisema lengo ni kuona kunakuwa na ustawi kwenye jamii kwa kuepuka maradhi hususani yanayohatarisha maisha ya watoto.

# Vyama vya ushirika vyaomba kupunguzwa utitiri wa tozo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WIZARA zinazosimamia ushirika zimeombwa kuandaa sera na sheria inayostawisha ushirika nchini, kwa kuondoa tozo nyingi zinazoelekezwa kwenye vyama vya ushirika.

Ombi hilo limetolewa na wadau wa ushirika wakati uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya chama cha kuweka na kukopa cha Lulu SACCOS cha jijini Mbeya, ambacho kimetumia Sh. milioni 16 kutoa misaada kwenye taasisi za umma na vituo vya kulelea watoto yatima mkoani Mbeya kama mchango wake kwenye jamii.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama, Meneja wa Lulu Saccos, Yacub Kiwambe, alisema chama chao kinawaomba viongozi wenye dhamana na ushirika kutoa elimu kwa wananchi ili kutambua umuhimu wa kujiunga kwenye vyama vya akiba na mikopo.

Alisema endapo serikali itaondoa utitiri wa kodi kutawawezesha wananchi wengi kujiunga kwenye ushirika na kupata fursa za kujikwamua kiuchumi.

"Tunaiomba serikali kuondoa baadhi ya tozo ambao zinatukandamiza kwa madai zinakwamisha jitihada za kujikwamua na umaskini kupitia utaratibu wa akiba ya kuweka na kukopa," alisema Kiwambe.

Mrajisi Msaidizi anayesimamia vyama vya kifedha nchini, Josephat Kisamalala, aliwataka viongozi kuendelea kuwa wabunifu kwa kutafuta vyanzo vingine vya fedha badala ya kuvibana vyama vya ushirika.

Mwenyekiti wa Bodi ya Lulu SACCOSS, Obeid Mtweve, alieleza fursa iliyopo nchini kwa wananchi kujiunga na vyama vya ushirika katika kujikwamua kiuchumi.

Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo, alisema serikali itaendelea kuimarisha usimamizi zaidi na udhibiti katika vyama vya ushirika kama nguzo ya maendeleo kwa wananchi.



# SMZ kuchunguza ubora wa bidhaa kwa viwango vya kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inafungua ukurasa mpya wa maendeleo kwenye uchunguzi wa ubora wa bidhaa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameyasema hayo jana wakati akizindua maabara mpya nne za kisasa za Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Maruhubi Mjini Unguja.

Alisema serikali ina nia ya dhati ya kulinda afya na usalama wa wananchi kwa kuchukua hatua stahiki za kupima ubora wa bidhaa zinazotumiwa nchini.

Dk. Mwinyi alisema taifa linashuhudia mafanikio makubwa ya utekelezaji wa malengo ya serikali baada ya uzinduzi wa maabara nyingine nne za vimelea, maabara ya vifungashio, nguo na ngozi.

Zingine ni maabara ya umeme yenye vifaa vya kisasa ambayo ina uwezo mkubwa wa kupima sampuli na kutoa majibu ya kuaminika kwa kutumia teknolojia za kisasa. "Ni matumaini yetu uwezo wa maabara hizi utaleta ufanisi wa haraka katika kupata majibu ya sampuli za bidhaa zinazoingizwa na zinazozalishwa nchini," alisema Dk. Mwinyi.

Akizungumzia suala la kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umaskini, Rais Dk. Mwinyi alisema suala hilo linakwenda sambamba na hatua ya kuimarisha maendeleo ya viwanda na biashara.

Alisema, moja kati ya tatizo kubwa iliyoikabili taasisi ya ZBS ni kutokuwapo kwa baadhi ya maabara zenye uwezo wa kupima sampuli za bidhaa na kupata matokeo kwa muda mwafaka.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema suala la viwango ni moja ya mazingira mazuri ya biashara Zanzibar.

Alisema Zanzibar haiwezi kufanya biashara kwa bidhaa zisizo na viwango na kuongeza kuimarika kwa maabara za ZBS ni moja ya maagizo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Shaaban alisema wizara imezindua mfumo wa kisasa utakaorahisisha maombi ya leseni za biashara kupitia teknolojia ya kisasa utakaojumuisha mamlaka 45 zinazotoa leseni na kuunganisha taasisi nyingine za serikali zinazotegemeana zitakazo fanyakazi pamoja.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yussuf Nassor Majid, alisema mbali ya mafanikio makubwa yaliyofikiwa na taasisi hiyo kwa kuzindua maabara nne za kisasa pia wanatarajia kuwa na kituo kikubwa cha ukaguzi wa magari kitakachokuwa na uwezo wa kukagua magari 150 kwa siku.

Alikitaja kituo hicho kitakuwa cha mfano kwa Afrika Mashariki na Kati pamoja na maabara ya vifaa vya ujenzi itakayofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) itakayokuwa na uwezo wa kupima vifaa vyote vya ujenzi vikiwamo nondo, kokoto, matofali, saruji, bati na vifaa vingine vya ujenzi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Shule ya Munduli, Wilaya ya Magharibi "A" jana, inayojengwa kwa fedha za mkopo wa ahueni ya Uviko-19. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Serikali inawajibu wa kujenga miundombinu imara, kisasa'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali ina wajibu wa kujenga miundombinu imara na ya kisasa inayoendana na wakati.

Amesema hali hiyo itasababisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo juzi wakati akikagua ujenzi wa Shule ya Munduli iliyoko Wilaya ya Magharibi "A" Unguja inayojengwa kwa fedha za UVIKO-19.

Alisema ni imani ya serikali kuwa mkandarasi ambaye anajenga shule hiyo atasimamia ujenzi huo kwa ufanisi ili kukamilisha mradi huo kwa viwango vinavyohitajika kwa wakati uliopangwa.

Hivyo alimtaka Kamishna wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Kanal Khamis Bakar, kusimamia mkataba wa ujenzi wa shule hiyo ili ikamilike kwa wakati.

Alieleza kuwa kukamilika kwa shule hiyo kutawasaidia walimu kufundisha katika mazingira mazuri na kujifunzia jambo ambalo litaongeza ufaulu wa wanafunzi hapa nchini.

Akigusia kuhusu suala la fedha za mradi huo, Hemed alisema serikali tayari ilishatenga fedha kwa ajili ya mradi huo na kuutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuhakikisha fedha hizo analipwa mkandarasi kwa mujibu wa utaratibu uliopo ili aweze kukamilisha ujenzi kwa wakati.

Pia aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa makandarasi wa ujenzi huo akisema ujenzi utakapokamilika watakaofaidika zaidi ni watu wa maeneo hayo na maeneo ya jirani.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohamed Mussa, alieleza kuwa wizara inaendelea kusimamia maendeleo ya ujenzi huo na kuhakikisha unakamilika kwa kiwango kinachokubalika. Kamishna wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Khamis Bakar Khamis, alisema ujenzi huo utaendelea vizuri na kuhidi majengo ya Shule ya Munduli kukamilika kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa.

# Waziri ataja sababu zinazokwamisha wabunifu kukosa haki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya Zanzibar kuwa na sheria tatu zinazohusiana na kulinda haki miliki na ubunifu, ukosefu wa sera na mikakati ya kulinda mali hizo kumetajwa kuwa ni chanzo kinachosababisha wabunifu kukosa haki zao.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Shaaban, aliyasema hayo juzi wakati akifungua warsha maalumu kwa watendaji na wadau wanaohusika na masuala ya ubunifu.

Alisema lazima nchi iwe na sera na sheria ya ubunifu ili kulinda kazi za wasanii.

"Kama nchi lazima tuwe na sera inayotupa mwelekeo wa jambo hili, tunataka wasanii wote waandike vitabu na mali kazi zao ziweze kulindwa na hiyo ndiyo mali bunifu na dunia ndiyo inakwenda huko tunapozungumza ubunifu wa viwanda," alisema.

Alisema Shirika la Mali Bunifu Duniani (WIPO) limeanza kuisaidia Zanzibar kutengeneza sera na mkakati wa taifa kulinda haki za watunzi na wabunifu kisiwani humo.

Mshauri Mwandamizi Divisheni ya Afrika kutoka WIPO, Loweta Asiedu, alisema siyo kawaida kuombwa na nchi kusaidiwa sera kama ilivyotokea kwa Zanzibar, hivyo kuwataka watendaji hao kuitumia fursa hiyo kwa umakini.

Kaimu Mkurugenzi Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, Rashid Masoud Othman, alisema lazima kuwapo na sera ya ubunifu ili kuwasaidia wajasiriamali na wabunifu. "Baada ya sera tutakuwa na ulinzi, kutakuwa na haki kama umebuni kitu hakuna mtu atakayejifanya ni chake na tumekuwa tukipokea malalamiko na kufanya majadiliano," alisema.

Mtaalamu wa mali bunifu hususani katika usajili wa alama za biashara, Murad Vellan alisema lengo ni kuhifadhi na kuzilinda haki za wabunifu wa mali na sanaa.

Alisema sera ikipatikana kutakuwa na ngao ya kuwalinda wabunifu ambao awali haki zao zilikuwa hazilindwi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL**
**FOR MARA**
**AT MUSOMA**
**MISCELLANEOUS APPLICATION NO. 05 OF 2023**
**WILLIAM GODFREY NYAKWIYESA.........APPLICANT**
**VERSUS**
**KWELWA HITLER............RESPONDENT**
**SUMMONS/ NOTICE**

**TO,**
**KWELWA HITLER (RESPONDENT)**

The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you particular of which are mentioned in a copy of the application which is obtainable from the registry of this tribunal. YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL in person (s) or by recognized agent(s) for mention on 03th April, 2023 at 08:00am in the forenoon.

**TAKE NOTICE THAT:**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.

Given under my hand seal of this Tribunal this 13th day of march, 2023.

Kitungulu, E.
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara

---

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL**
**FOR MARA**
**AT MUSOMA**
**MISCELLANEOUS APPLICATION NO. 04 OF 2023**
**KITANDA MKIRYA MWAMBARA........APPLICANT**
**VERSUS**
**KWELWA HITLER............RESPONDENT**
**SUMMONS/ NOTICE**
**TO,**
**KWELWA HITLER (RESPONDENT)**

The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you particular of which are mentioned in a copy of the application which is obtainable from the registry of this tribunal. **YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL** in person (s) or by recognized agent(s) for mention on 03th April, 2023 at 08:00am in the forenoon.

**TAKE NOTICE THAT:**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.

Given under my hand seal of this Tribunal this 13th day of march, 2023.

Kitungulu, E.
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU DIOCLES ALEXANDER MUGANGUZI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA GARI AINA YA TOYOTA HIACE LENYE NAMBA ZA USAJILI T103 BMV. AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA KAG/BUK/RB/97790/2023. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE AU **APIGE SIMU NAMBA 0629758887**

---

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No.28 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late of the late ERICK JOSIA LYIMO**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by EVANCE ERICK LYIMO.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 4 Day of 4, 2023

**Dated at Dodoma this 13 day of 3, 2023.**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**MAOMBI YA RUFAA NA. 27 YA 2022**
**SILVESTER JOB CHIPONDO ......MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**AGNESS CHARLES ERNEST......MJIBU MAOMBI**
**KWA: AGNESS CHARLES ERNEST**
**POPOTE PALE ALIPO.**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA MAOMBI YA RUFAA NA.27/2022 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya MHE. JAJI MASAJU, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Jumanne tarehe 25/04/2023.

HIVYO unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

NA ENDAPO; Hautafika wewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

IMETOLEWA kwa mkono wangui na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 14/03/2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU DODOMA

---

## TANGAZO OFA YA KIWANJA

**Lugendo Isaac Msegu na Laura Mahava Msegu**

Wanatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba 76 Kitalu "MM" Low Density kilichopo Lubaga Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Lugendo Isaac kwa **Simu namba 0622-279888.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LILIAN MOSES KIMARO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI (TOYOTA RAV 4) YENYE NAMBA ZA USAJILI T336 DQF MALI YA KAMPUNI YA ONE ACRE TANZANIA LTD. CHASIS NAMBA: SXA160021014. ENGINE NAMBA: 3S7360104. KADI NAMBA: 8023977. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI RB **NAMBA IRI/IRI/RB/97000/2023.**

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**DENICE SPEAK KAMUGISHA** natangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index No. S.1071/0332 Kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia ST. MATHEW'S SECONDARY SCHOOL mwaka 2014.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi: **DAR/MBA/RB/60497/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB. NA. MMC/LD/2000**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: BENNY BARNABA ZILLINDE WA S.L.P 100075, DAR ES SALAAM.**
**ARDHI: KIWANJA NA. 284 KITALU 5 KICHANGANI MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: ERICA BARNABAS ZILLINDE WA S.L.P 100075 DAR ES SALAAM AMBAE NI MNUFAIKA WA MALI KWA MUJIBU WA MIRATHI NAMBA 393/2016 ILIYOTOLEWA MAHAKAMA YA MWANZO MBAGALA DAR ES SALAAM.**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa SIKU 30 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA-MOROGORO S.L.P166 MOROGORO**

Valency H.K
**KNY:MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO**

Valency H.K
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

Kny MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MOROGORO**
**SHAURI LA UTEKELEZAJI MADAI 29 YA 2022**
**HADSON JACKSON MUHILA NA WENZAKE WAWILI....WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**PICADILLY CONSTRACTION LTD...MDAIWA**

**WITO WA MAHAKAMA**

**KWA: PICADILLY CONSTRACTION LTD**

**Wito huu ni wa kesi tajwa hapo juu,** ambayo imepangwa kusikilizwa tarehe21 mwezi wa 03 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa Naibu msajili A.W Mmbando.

Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili au mtu yeyote aliyeidhinishwa kusimama kwa niaba yako na pia unatakiwa kutoa maelezo yako siku hiyo na nakala zote za ushahidi utakaotumia kwa shauri hili.

**Zingatia kwamba**, Kutohudhuria siku ya kesi na kwa kwa wakati uliotajwa hapo juu, mahakama itaendelea kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako.

Imetolewa chini ya muhuri wa mahakama kuu kanda ya Morogoro leo siku ya tarehe 08 mwezi 03 mwaka 2023.

---

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KITUO CHA MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 33/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU RITA ATILIO SENG'INGO WA MISONGENI**
**KATIKA SHAURI LA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ROMANUS ATILIO MWANG'NDO**

**TANGAZO**
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20/ Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 03 mwaka 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GERALD NATHANIEL MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 766 AGJ.** **ENGINE NO. 2Y6718685** **CHASSIS NO. YN850086729** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi**. Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/241973/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JONATHAN ESTOMIH MADOM** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 546 ADV – MERCEDES BENZ. CHASSIS NAMBA WDB1240202A167214. ENGINE NAMBA 10292222006405. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/98676/2023.**

---


***OFISI ZA MATANGAZO***

***Mikocheni Industial Area,***

***Po.Box 31042, Dar es Salaam.***

***Mobile: +255 - 745 700 710.***

***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***

***Website: www.ippmedia.com***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0677020701***


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mtoto wa Museven atangaza kuwania urais Uganda 2026

**KAMPALA, Uganda**

MTOTO wa Rais Yoweri Museven wa Uganda, ametangaza kugombea kiti cha urais mwaka 2026.

Jenerali Muhoozi Kainerugaba, ambaye anasifika kwa kuwa na kauli zenye utata na zenye kuibua mijadala ametoa tangazo hilo kupitia ukurasa wake wa Twitter juzi Jumatano.

Katika ujumbe huo, Kainerugaba, alisema watu wamekuwa wakimtaka atoe msimamo wake kuhusu kiti cha urais.

"Mmenitaka mimi kulisema daima! Sawa, kwa jina la Yesu Mungu wangu, kwa jina la vijana wote wa Uganda na dunia na kwa jina la mageuzi bora, nitagombea Urais katika mwaka 2026!" aliandika Twitter.

Awali mkuu huyo wa zamani wa Jeshi la Ardhini la Uganda, aliweka nia ya kumrithi Baba yake kiti cha urais wa Uganda, lakini hakutaja wakati gani atafanya hivyo.

Alisema viongozi wengi mashuhuri akiwamo aliyekuwa rais wa Cuba, Fidel Castro, aliingia madarakani akiwa na umri wa miaka 32, tofauti na yeye ambaye amebakisha mwaka mmoja kufikia 50.

Alisema jambo hilo siyo sawa kwani vijana wanapaswa kuwa viongozi wa mataifa yao, badala ya wazee wanaoongoza.

"Fidel Castro Shujaa wangu alikuwa Rais akiwa na umri wa miaka 32, mimi ninakaribia kufikia miaka 49, sio sawa kabisa (Kutokuwa Rais), vijana wanapaswa kuwa marais wa Mataifa yao" alisisitiza katika ujumbe huo.

Aliongeza kwa kuwataka vijana kutokubali kuongozwa na wazee, ni dhahiri wakati wa vijana kuwa madarakani umefika ni muhimu kutimiza kwa vitendo.

"Nani anakubaliana na mimi kwamba muda wetu Vijana umewadia?, Inatosha sasa kuendelea kuongozwa na Wazee na kututawala, ni muda wa vijana kung'aa," aliandika.

Alitolea mifano viongozi waliopata madaraka wakiwa vijana ni Waziri Mkuu wa Uingereza, mwenye miaka 42 na Waziri Mkuu wa Finland ana miaka 37, hivyo amechoka kusubiri.

"Sisi wengine tunakaribia miaka 50, tumechoka kusubiri, nitasimama kugombea" alimalizia kwa kusisitiza.

*BBC*



Raia wa Korea ya Kusini akipita karibu na skrini ya runinga inayoonyesha matangazo ya habari yenye kanda ya jaribio la kombora la Korea Kaskazini, kwenye kituo cha reli mji mkuu wa Seoul jana. **PICHA: AFP**

# Rais Ruto amuonya Odinga kuitisha maandamano J'tatu

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya William Ruto, amemuonya kiongozi wa upinzani Raila Odinga, kuhusu kuandaa maandamano ya umma yaliyopangwa kufanyika Jumatatu ijayo.

Kiongozi huyo aliapa kutoruhusu Odinga kufanya maandamano ambayo yatahatarisha maisha ya Wakenya,uharibifu wa mali au kulemaza shughuli za biashara.

Alisema Kenya ni nchi inayoongozwa kwa misingi ya sheria na hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kuzivunja.

Odinga alitangaza kuwa Machi 20, itakuwa siku ya mapumziko nchini humo ili kuruhusu watu kushiriki maandamano ya kupinga utawala wa Rais Ruto.

Hata hivyo, Waziri kiongozi Musalia Mudavadi, amekosoa tangazo hilo akisema linakiuka katiba ya nchi, kwani Odinga hana mamlaka ya kutangaza mapumziko ya kitaifa.

Kiongozi huyo wa upinzani ameendelea kusisitiza hatambui uongozi wa Ruto tangu alipotangazwa mshindi wa uchaguzi wa Rais uliofanyika Agosti mwaka jana.

Odinga alidai uchaguzi huo ulitawaliwa na udanganyifu wa kura na kutaka Tume huru ya uchaguzi kutathminiwa upya licha ya mahakama ya juu kuthibitisha ushindi wa Rais Ruto.

Tayari,kaunti kadhaa nchini Kenya katika kipindi cha siku chache zilizopita, zimeshuhudia maandamano ya umma wakiitikia wito wa Odinga wa kuipinga serikali.

Miongoni mwa kaunti hizo ni Migori na Kisumu ambazo ni ngome za kisiasa za kiongozi huyo mkuu wa upinzani.

Viongozi wa muungano wa Azimio, wanafanya mikutano ya hadhara nchini , kuwashawishi wafuasi wao kugoma na kuipinga serikali kwa kile wanachokitaja kushindwa kushughulikia tatizo la ugumu wa maisha,kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu,ajira na ufisadi.

*BBC*

## Poland yadai kukamata majasusi wa Russia

**WARSAW, Poland**

WATU kadhaa raia wa kigeni wamekamatwa nchini Poland baada ya kushukiwa kuifanyia ujasusi Russia.

Maofisa wawili wa serikali ya Poland wameiambia BBC, baada ya kituo cha redio RMF FM kiliripoti kwamba huduma za usalama za Poland zimevunja mtandao unaoifayia kazi Russia.

Watu sita walikamatwa kwa kushukiwa kuweka kamera za siri za kupiga picha za video miundo mbinu ya usafiri unaotumiwa kusafirisha misaada kwenda nchini Ukraine.

RMF FM ilisema kuwa kikundi hicho kilikuwa kimeandaa mipango ya hujuma.

Mzozo wa kufanyiana ujasusi wa muda mrefu kati ya nchi ya Russia na zile za Magharibi umeimarika tangu kuanza kwa vita ya Ukraine.

Poland ni mojawapo ya washirika wakuu wa Ukraine, vikosi vyake vimekuwa vikiwakamata watu kadhaa wanaoshukiwa kufanya ujasusi kwa ajili ya Russia.

Kulingana na kituo hicho cha redio, kikundi hicho cha majasusi kilikuwa kimeweka kamera za video CCTV kando ya makutano ya njia ya reli na barabara muhimu ya usafirishaji iliyoko katika jimbo la Podkarpackie , inayopakana na Ukraine.

Baadhi ya kamera hizo zilizopatikana zimewekwa karibu na kiwanja kidogo cha mkoa cha ndege ambacho kimegeuzwa kuwa cha kimataifa kwa ajili ya kusafirisha misaada ya kijeshi na ya kibinadamu kwenda nchini Ukraine.

Wakati huo huo, Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, ametangaza nchi yake itapeleka silaha zaidi nchini Ukraine.

Scholz aliyasema hayo bungeni jana alipowasilisha taarifa ya serikali kuhusu mkutano wa kilele wa Umoja wa Ulaya utakaofanyika wiki ijayo.

Alisema pamoja na washirika wake wa Ulaya, Ujerumani itahakikisha kwamba Ukraine inapokea silaha na vifaa vya kujilinda.

Ujerumani tayari inatoa msaada mkubwa wa silaha kwa Ukraine, kwa ajili ya kuzuia mashambulizi ya Russia.

Viongozi 27 wa Umoja wa Ulaya watajadili masuala ya ushindani wa kibiashara, nishati, na vita vya Ukraine, wakati watakapokutana mjini Brussels nchini Uholanzi wiki ijayo.

*DW*

# MFAUME, PIALALI KURUDIANA SEPTEMBA, TAMBO ZATAWALA

**Na Saada Akida**

MABONDIA wa ngumi za kulipwa nchini wenye uhasimu mkubwa, Idd Pialali na Mfaume Mfaume wamesaini mkataba wa kushiriki pambano la marudiano litakalofanyika Septemba Mosi, mwaka huu, imefahamika.

Pialali na Mfaume wamesaini mkataba huo juzi katika hafla maalumu iliyofanyika kwenye viwanja vya Leaders Club, Dar es Salaam juzi huku kila mmoja akitamba kumaliza pambano hilo mapema.

Pambano hilo litaandaliwa na Kampuni ya Posh Queen Boxing Promotion na litajulikana kwa jina la King Of The Night, kwa sababu linabeba hisia za mashabiki wengi wa ngumi baada ya lile la awali lililofanyika Arusha kuvunjika.

Akizungumza na gazeti hili, Mfaume alitamba atahakikisha anamchakaza mpinzani wake mapema na kama haitakuwa hivyo basi ataacha mchezo wa ngumi.

"Fanya mazoezi kwa bidii halafu kasema raundi ya tatu mwisho, huyu asipoamkia ICU (chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum), naacha boxing. Mama Mfaume kaongea na timu yangu timu ya Mabibo siongei sana, nasemaje tupigane mpaka mmoja afe," alisema Mfaume.

Aliongeza pambano la awali lilivunjwa na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), kutokana na Piarali kupata jeraha juu ya paji la uso, sasa hivi wanahitaji matokeo ya kweli.

Pialali alisema mwanaume haongei sana na anafanya vitendo, yuko tayari kupambana na Mfaume katika pambano hilo la marudiano na atahakikisha 'anamkalisha' chini.

"Huyu (Mfaume) sio bondia, sasa dawa yake nishaipata tayari, kuna watu anawategemea lakini nampiga 'knockout' mbaya sababu sio bondia, hamalizi huyu hana maajabu," alisema na aliongeza;

Mfaume kampiga nani hapa Tanzania? Sisi tunacheza ngumi hatuogopi, kazi anayo, Manzese msiwe na presha, hapa anajikaza tu ila tutampiga," alitamba Pialali.

Pambano hilo litakuwa la raundi 10 kama lile la Desemba 26, mwaka jana ambalo lilivunjika katika raundi ya kwanza baada ya kutafsiriwa mabondia hao waligongana vichwa na kusababisha Pialali kupasuka usoni.



Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo (mwenye kofia), akimwelekeza jambo Charles Mkwasa 'Master' katika kozi ya maboresho ya CAF A Diploma inayoendelea jijini, Tanga. Kushoto ni Jamhuri Kihwelo 'Julio' na Mecky Maxime ambao pia wanashiriki kozi hiyo. **PICHA: TFF**

# Chana awaita Wa-asia kuwekeza

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi, Pindi Chana, ameikaribisha jamii ya watu wa India kuwekeza katika sekta tofauti hapa nchini ikiwamo michezo.

Chana alitoa kauli hiyo katika sherehe za Holi Milan 2023 ambazo husherehekewa na jamii hiyo kwa kupaka rangi kavu au ya maji pamoja na kuimba na kucheza.

Sherehe hizo ziliandaliwa na Kituo cha Utamaduni wa India, Swami Vivekananda (SVCC) kwa kushirikiana na Ubalozi wa India na kuhudhuriwa na mabalozi wanaowakilisha nchi mbalimbali zikiwamo Nigeria, Vietnam na Korea Kusini.

Chana aliwaomba waendelee kukuza ushirikiano katika kuimarisha sekta ya utamaduni, sanaa na michezo.

"Serikali inazidi kuwaalika diaspora waliopo duniani kote, wanaotoka India kuja kuwekeza Tanzania, tufanye kazi kwa pamoja tushirikiane, milango iko wazi," aliwakaribisha.

Mkurugenzi wa Kituo cha SVCC, Dkt. Soumya Chavan, alisema wameungana na wenzao ulimwenguni kusherehekea Holi kwa kujumuisha makundi yote, watoto, vijana, watu wazima na wazee.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, alisema sherehe za Holi ni tukio muhimu linalosherehekewa ulimwengu kwa kukutanisha watu pamoja.

## Ngome kucheza Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mundu FC, Ngome imefikisha pointi 60 na kuungana na New City kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu ya Zanzibar katika msimu ujao.

Kocha Msaidizi wa Ngome, Suleiman Mohamed 'Mo', alisema wamefurahi kuona timu hiyo inafanikiwa kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu Zanzibar kwa mara ya kwanza.

Kocha huyo alisema kiu yao kubwa ilikuwa ni kucheza Ligi Kuu Zanzibar na watajipanga kufanya maandalizi mapema ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika ligi hiyo.

"Tumepanda daraja, hakika tulipigana vita mpaka tulifika wakati tuliona kupanda daraja hatutaweza kutokana na ugumu wa ligi, lakini wachezaji walijituma mpaka dakika ya mwisho tumefanikiwa," Mo alisema.

Aliwapongeza wachezaji na mashabiki wao waliohakikisha timu hiyo inapata mafanikio ambayo yataendelea kukumbukwa wakati wote.

## Singida BS yawaza kutinga fainali FA

**Na Hadija Mngwai**

SINGIDA Big Stars imetamba inajipanga kuhakikisha inatinga hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA au kulibeba taji hilo licha ya ushindani uliokuwapo katika michuano hiyo.

Singida Big Stars itacheza mechi ya hatua ya robo fainali dhidi ya Mbeya City, wakati Simba wataikabili Ihefu huku Yanga ikiwavaa Geita Gold na Azam FC itakipiga na Mtibwa Sugar.

Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, aliliambia gazeti hili wanafahamu ugumu wa michuano hiyo, lakini namna walivyojipanga wanaamini watafikia malengo yao.

"Tunafahamu tumeingia hatua ya robo fainali yenye ushindani sana, timu zote zilizoingia hatua hii ni bora zinafanya vizuri kwenye ligi. Mbeya City ni mpinzani mkubwa sana na tunaenda kukutana nae tukiwa hatuna shaka hata kidogo," alisema Massanza.

Aliongeza kwa sasa kila timu inajiimarisha na wao wanatarajia kuweka rekodi ya kushinda kombe hilo wakiwa wanashiriki kwa mara ya kwanza michuano hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OFA NONO KWA MESSI
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35, atapewa ofa ya euro milioni 220 kwa mwaka ili kuhamia klabu ya Saudi Arabia baada ya mkataba wake na Paris St-Germain utakapokamilika msimu wa joto. ***(Marca)***

### ALVAREZ KUZEEKEA CITY
MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Julian Alvarez, mwenye umri wa miaka 23, anatazamiwa kusaini mkataba mpya ambao utamweka mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Argentina hapo Etihad hadi kufikia mwaka 2028. ***(Mail)***

### POGBA KUBAKIA JUVENTUS
KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba, anataka kubakia Juventus msimu ujao, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kucheza kwa dakika 35 tu kwenye Ligi ya Serie A msimu huu kwa sababu ya majeraha. ***(90 Min)***

### GUNDOGAN ANUKIA BARCA
KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, tayari amezungumza na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32, kuhusu uhamisho. Mkataba wa Gundogan na klabu yake ya Manchester City unamalizika majira ya joto. ***(AS)***

### DORTMUND KUMBANA BRANDT
KLABU ya Borussia Dortmund huenda ikampa mkataba mpya winga wa kimataifa wa Ujerumani, Julian Brandt, mwenye umri wa miaka 26 ikiwa ni jitihada za kuzuia nia ya Arsenal na Tottenham Hotspur kumnasa. ***(Bild)***

### MUANI ATAKIWA UNITED
KLABU ya Manchester United inaweza kuwasilisha ofa ya pauni milioni 105 kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Randal Kolo Muani, mwenye umri wa miaka 24. ***(Sport Bild)***

### KANE AWINDWA ULAYA
CHELSEA imeonyesha nia ya kumsajili Manu Kone wa Borussia Monchengladbach huku kiungo huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa mwenye umri wa miaka 21 akiivutia pia Paris St-Germain. ***(Sun)***

### LOFTUS-CHEEK KUUZWA
CHELSEA iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa kimataifa wa England, Ruben Loftus-Cheek, mwenye umri wa miaka 27 msimu huu wa joto na klabu tano za Ligi Kuu England pamoja na AC Milan na AS Roma zinamwania. ***(Football Insider)***

### BENZEMA, MADRID SAFI
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Karim Benzema, mwenye umri wa miaka 35 ameripotiwa kukubali kusaini mkataba mpya na vigogo wa Hispania, Real Madrid. ***(L'Equipe)***

### FULLKRUG ANUKIA EPL
KLABU ya West Ham inajipanga kumnunua mshambuliaji wa Werder Bremen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Niclas Fullkrug, mwenye umri wa miaka 30. ***(Sport Bild via Sport Witness)***

### GUERREIRO AGEUKA LULU
KLABU za Newcastle, Aston Villa, Wolves na Leeds zinachuana kuwania saini ya beki wa pembeni wa kimataifa wa Ureno, Raphael Guerreiro, mwenye umri wa miaka 29 mara mkataba wake na Borussia Dortmund utakapokamilika msimu wa joto. ***(90min)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ANCELOTTI: VINICIUS NDIYE NYOTA BORA ZAIDI DUNIANI

●●●Kocha huyo asema Mbrazil huyo amekuwa katika kiwango cha juu kuanzia...

**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema Vinicius Junior, ndiye mchezaji "bora zaidi duniani" baada ya kuwasaidia Los Blancos hao kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Liverpool hapo juzi.

Mbrazil huyo alitoa pasi ya bao la ushindi lililofungwa na Karim Benzema, dakika ya 78 katika mchezo wa mkondo wa pili wa hatua ya 16 bora, akiwa amefunga mara mbili na kutengeneza jingine katika ushindi wa magoli 5-2 wa mkondo wa kwanza kwenye Uwanja wa Anfield wiki tatu zilizopita.

Ancelotti alisema Vinicius alikuwa "mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani" kabla ya pambano lao la Copa del Rey dhidi ya Barcelona mapema mwezi huu, na sasa haoni mtu bora zaidi.

"Kwangu mimi, yeye ndiye bora zaidi duniani," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.

"Leo (juzi) hakufunga, lakini alicheza vizuri sana na kutoa bao."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil amefunga mabao 19 msimu huu, pamoja na kutoa asisti 10.

Vinicius ni mmoja wa wachezaji wawili pekee waliofunga na kusaidia mabao 10 (mabao 13 na pasi 10 za mabao) akipitwa na Kylian Mbappe (mabao 21 na asisti 11).

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alifurahia msimu mzuri wa 2021-22 akiwa na mabao 17 ya LaLiga na 22 katika mashindano yote akiwa na Los Blancos huku wakishinda ligi na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili.

Vinicius alimaliza wa nane katika upigaji kura wa Ballon d'Or mwaka jana, alishinda mchezaji mwenzake Benzema, huku akishika nafasi ya 11 kwa tuzo ya Mchezaji Bora wa FIFA wa Wanaume iliyochukuliwa na Lionel Messi mwezi uliopita.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,090,5
MECHI KALI
NOTTINGHAM
VERSUS
NEWCASTLE
1 | 4.81
X | 3.61
2 | 1.65
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LIVERPOOL TUNAPAMBANIA KUMALIZA 4 BORA - KLOPP



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema kuondolewa kwa Liverpool katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kumewapa "kazi kubwa" kuokoa msimu wao kwenye Ligi Kuu England na kocha huyo anaamini mechi tatu ndani ya wiki dhidi ya Manchester City, Chelsea na Arsenal zitawapa au kuvunja matumaini yao.

Bao la Karim Benzema kipindi cha pili, bao lake la 13 katika mechi nane zilizopita za mtoano za Ligi ya Mabingwa Ulaya lilitosha kupata ushindi wa bao 1-0 na wa hatua ya 16 bora, ikipata ushindi wa jumla ya magoli 6-2.

Kuondolewa mapema kwa Liverpool kwenye kinyang'anyiro hicho kunamaanisha hawawezi kushinda tena taji msimu huu na kwa sasa wakiwa katika nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu England, nafasi yao pekee waliyonayo ni kumaliza katika nne bora.

Wakiwa na Tottenham walio katika nafasi ya nne kwa pointi sita mbele ya Liverpool, na Newcastle United pointi mbili mbele ya washindi wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya 2022 wakiwa na mchezo mkononi, Klopp alikiri wachezaji wake lazima wazingatie kumaliza nafasi ya nne.

"Tunataka kuwa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kila mwaka na ni kazi kubwa kwetu kumaliza nafasi ya nne na tunajua hilo," alisema Klopp.

"Baada ya mapumziko ya kimataifa, tuna wiki ifaayo mbele yetu, City, Chelsea na Arsenal. Labda hiyo itafafanua kile tunachopata msimu huu.

# Osimhen anaamini Napoli itabeba Uefa

**NAPLES, Italia**

VICTOR Osimhen anaamini Napoli wako imara na wanatosha kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufika robo fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza kwa ushindi mnono dhidi ya Eintracht Frankfurt.

Osimhen alifunga mara mbili wakati Napoli ikishinda mabao 3-0 katika mechi ya mkondo wa pili wa hatua ya 16 bora iliyochezwa kwenye Uwanja wa Diego Armando Maradona juzi, na kupata mafanikio ya jumla ya mabao 5-0 dhidi ya washindi wa Ligi ya Europa msimu uliopita.

Piotr Zielinski pia alifunga kwa penalti huku Napoli ikiandika ushindi wa nne katika mechi nyingi za Ligi ya Mabingwa Ulaya nyumbani msimu huu.

Huku Napoli ikiwa na jumla ya mabao 26 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo haijalinganishwa na timu nyingine yoyote msimu huu, Osimhen anaamini viongozi hao Serie A wanaweza kubeba taji hilo la Ulaya.

"Nadhani lolote linawezekana na tuna kikosi cha kufikia ndoto hii," alisema Osimhen akiiambia BT Sport.



HABARI MICHEZO

583,531/-

# JULIO AIFUNDA SIMBA ILI KUIMALIZA HOROYA

**Na Hadija Mngwai**

ALIYEKUWA Kocha wa Simba, Jamhuri Kihwelo 'Julio' (pichani), ametoa somo kwa nyota wa timu hiyo kutobweteka katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Simba inahitaji ushindi ili kujisafishia njia ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na Nipashe, Julio, alisema Simba inahitaji kuweka mikakati imara na kamwe wasiingie uwanjani wakiwa na mawazo ya ushindi waliopata kwenye mechi ya nyumbani na ugenini dhidi ya Vipers.

Julio alisema wanatakiwa wapambane kwa sababu bado hawajamaliza kazi iliyoko mbele yao.

"Tulianza kwa kupoteza michezo miwili na kushinda michezo miwili kwa maana hiyo tupo nusu kwa nusu, tunahitaji tushinde dhidi ya Horoya ambayo kwangu mimi sio mechi rahisi. Horoya ikitufunga safari itakuwa imeishia hapo, kama unavyojua mpira wa sasa hivi unashinda popote na unafungwa popote.

Tunahitaji kuweka mikakati madhubuti na kudhamiria, kuwa kitu kimoja kuanzia kwa wanachama, viongozi na wachezaji wenyewe, hatua ya makundi haina tofauti na mtoano, hivyo unahitaji ushinde ili usonge mbele, wachezaji wajitume wasibweteke," alisema Julio.



Baada ya mechi hiyo, Simba itasafiri kwenda Morocco kuwafuata Raja Casablanca ambayo tayari imeshafuzu hatua ya robo fainali baada ya kushinda mechi zake zote nne ilizocheza.

# Yanga : Tutaiduwaza US Monastir

INATOKA UK. 24

kwenda Lubumbashi kuwafuata TP Mazembe katika mechi ya mwisho huku wakiwa na kumbukumbu ya kuwafunga Wakongomani hao mabao 3-1 katika mchezo wa kwanza uliofanyika hapa nyumbani.

Yanga na Simba wanaogelea bahari ya fedha za Rais Samia aliyeahidi kununua kila bao litakalofungwa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika kwa gharama ya Sh. milioni tano.

Nafasi ya pili katika Kundi D inashikiliwa na Yanga yenye pointi saba ikifuatiwa na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), yenye pointi tatu huku Real Bamako ya Mali yenye pointi mbili ikishika mkia katika kundi hilo.

# Simba yakamilisha hesabu za Horoya

INATOKA UK. 24

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mchezo wa kesho ni muhimu sana kwao na wanawaomba mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Mkapa ili kuwasapoti vijana wao.

"Mchezo wa Jumamosi dhidi ya Horoya AC ni muhimu na mgumu, tunajua kama tutajitokeza mashabiki 60,000 kwa Mkapa, Horoya AC hata wawe bora vipi hawatoki, Wanasimba kutoka kila maeneo yote



ya hapa nchini mnatakiwa kujitokeza uwanjani ili timu itinge robo fainali," alisema Ahmed.

Aliongeza itakuwa fedheha kubwa endapo watashindwa kuifunga Horoya na kuishia hatua ya makundi.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.18/03/23 | 18:00 | Aberdeen FC vs Heart of Midlothian FC | 2.38 | 3.40 | 2.65 |
| 02.18/03/23 | 18:00 | Rotherham United vs Cardiff City | 2.55 | 3.15 | 2.65 |
| 03.18/03/23 | 18:00 | Stoke City vs Norwich City | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 04.18/03/23 | 18:15 | Albacete Balompie vs Granada CF | 2.55 | 2.95 | 2.80 |
| 05.18/03/23 | 18:30 | Portimonense SC vs FC Vizela | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 06.18/03/23 | 20:30 | Espanyol Barcelona vs RC Celta de Vigo | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 07.18/03/23 | 20:45 | FC Emmen vs Sparta Rotterdam | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 08.18/03/23 | 21:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs FC Metz | 2.60 | 2.95 | 2.75 |
| 09.18/03/23 | 21:00 | Chamois Niort FC vs Stade Lavallois MFC | 2.60 | 3.00 | 2.70 |
| 10.19/03/23 | 14:15 | FC Groningen vs SC Heerenveen | 2.70 | 3.20 | 2.46 |
| 11.19/03/23 | 14:30 | Sampdoria Genoa vs Hellas Verona | 2.85 | 3.00 | 2.48 |
| 12.19/03/23 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Hannover 96 | 2.46 | 3.30 | 2.65 |
| 13.19/03/23 | 16:30 | Excelsior Rotterdam vs SC Cambuur | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 14.19/03/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Stade Brest 29 | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 15.19/03/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Villarreal CF | 2.90 | 3.05 | 2.40 |
| 16.19/03/23 | 19:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.40 | 3.15 | 2.45 |
| 17.19/03/23 | 20:00 | Lazio Rome vs AS Roma | 2.60 | 2.95 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 17/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4922 | FC Metalist Kharkiv vs Oleksandria | 3.65 | 3.24 | 1.89 |
| 15:00 | 3898 | FC Olimpik vs Otmk Olmaliq | 3.02 | 3.07 | 2.20 |
| 15:15 | 5628 | Sabah vs Penang | 1.30 | 4.72 | 7.60 |
| 16:00 | 5020 | Selangor FC vs Johor Darul Takzim | 5.53 | 4.05 | 1.47 |
| 16:00 | 5900 | Al-Merrikh vs Esperance Tunis | 3.86 | 2.93 | 1.96 |
| 16:30 | 2214 | CS Sfaxien vs Africain | 2.40 | 2.55 | 3.33 |
| 16:45 | 5395 | City Football Club vs Masafi | 4.32 | 3.65 | 1.65 |
| 17:00 | 2256 | MC Oran vs CS Constantine | 3.10 | 2.65 | 2.28 |
| 17:00 | 4294 | Al-Shamal vs Al Sadd SC | 7.00 | 4.94 | 1.31 |
| 17:00 | 4570 | US Biskra vs RC Arbaa | 1.90 | 3.01 | 4.15 |
| 17:00 | 5343 | FK Panevezys B vs FK Babrungas Plunge | 2.87 | 3.53 | 2.09 |
| 17:30 | 4167 | Pakhtakor vs Navbahor Namangan | 1.78 | 3.23 | 4.21 |
| 18:00 | 1569 | Partizan vs Radnik Surduluca | 1.20 | 5.30 | 11.21 |
| 18:00 | 1752 | FC Minsk vs Slavia Mozyr | 2.75 | 3.42 | 2.25 |
| 19:00 | 3055 | Vsnk Varazdin vs HNK Gorica | 1.99 | 3.24 | 3.34 |
| 19:00 | 4359 | Cotonsport vs Al Ahly Cairo | 5.00 | 3.80 | 1.48 |
| 19:30 | 1708 | Al Dhafra vs AL Wahda Scc (UAE) | 7.37 | 4.61 | 1.32 |
| 19:30 | 5423 | Al Ain vs Al Nasr Dubai | 1.37 | 4.42 | 6.58 |
| 20:00 | 3510 | Konyaspor vs Galatasaray | 3.98 | 3.67 | 1.78 |
| 20:00 | 3769 | Cork City vs Shelbourne | 2.41 | 2.93 | 2.82 |
| 20:00 | 4235 | Shamrock Rovers vs St Patricks | 1.69 | 3.49 | 4.31 |
| 20:00 | 5213 | FK Mladost Gat vs FK Radnicki 1923 | 2.88 | 2.93 | 2.37 |
| 20:00 | 5299 | Altinordu vs Tuzlaspor | 2.40 | 3.19 | 2.63 |
| 20:10 | 1582 | SKN St Polten vs FC Liefering | 2.03 | 3.42 | 3.16 |
| 20:10 | 4766 | Kapfenberg vs Sturm Graz II | 3.32 | 3.58 | 1.93 |
| 20:30 | 3502 | Sassuolo vs Spezia | 1.76 | 3.69 | 3.99 |
| 20:30 | 3615 | Stellenbosch vs Amazulu | 2.28 | 2.88 | 3.29 |
| 20:30 | 4515 | Moroka Swallows FC vs Golden Arrows | 2.50 | 2.87 | 2.93 |
| 21:00 | 2790 | Wexford Youths vs Kerry FC | 1.25 | 5.16 | 8.67 |
| 21:30 | 5970 | Yverdon-Sport FC vs FC Schaffhausen | 1.84 | 3.59 | 3.49 |
| 22:00 | 1023 | FC Volendam vs Fortuna Sittard | 2.45 | 3.36 | 2.61 |
| 22:00 | 4400 | CR Belouizdad vs Zamalek | 2.02 | 2.92 | 3.69 |
| 22:00 | 5156 | Jong Ajax vs Almere City | 2.91 | 3.74 | 2.07 |
| 22:00 | 5382 | PEC Zwolle vs NAC Breda | 1.33 | 4.98 | 7.06 |
| 22:15 | 2471 | FC Wil vs FC Aarau | 1.92 | 3.51 | 3.30 |
| 22:30 | 1232 | Monchengladbach vs Werder Bremen | 1.90 | 3.66 | 3.46 |
| 22:45 | 2159 | Atalanta vs Empoli | 1.43 | 4.39 | 6.19 |
| 22:45 | 3768 | Bohemians FC vs UCD Dublin | 1.24 | 5.05 | 9.69 |
| 22:45 | 4184 | Derry City vs Sligo Rovers | 1.46 | 3.86 | 5.97 |
| 22:45 | 4530 | Athlone Town vs Treaty United | 2.24 | 3.32 | 2.76 |
| 22:45 | 4716 | Sheffield Wed vs Bolton | 1.74 | 3.64 | 4.35 |
| 22:45 | 4753 | Arbroath vs Morton | 2.60 | 3.12 | 2.56 |
| 22:45 | 5054 | Cercle Brugge vs Racing Genk | 2.92 | 3.38 | 2.24 |
| 22:45 | 5399 | Larne vs Ballymena Utd | 1.15 | 5.97 | 13.38 |
| 23:00 | 3826 | Lyon vs Nantes | 1.62 | 3.85 | 4.70 |
| 23:00 | 4036 | Valladolid vs Athletic Bilbao | 3.50 | 3.30 | 1.99 |
| 23:00 | 4973 | Nottingham vs Newcastle | 4.81 | 3.61 | 1.65 |
| 23:00 | 5799 | Malaga vs Levante | 3.89 | 3.24 | 1.91 |
| 23:15 | 1911 | Santa Clara vs Rio Ave | 2.62 | 2.97 | 2.72 |
| 23:30 | 5778 | Sport Boys Association vs Deportivo Garcilaso | 2.22 | 3.28 | 2.82 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Machi 17, 2023
Nipashe



## Ancelotti: Vinicius ndiye nyota bora zaidi duniani

UKURASA 21

# YANGA SC : TUTAIDUWAZA US MONASTIR JUMAPILI

●●●Yafunguka mamilioni ya Rais Samia yameongeza ari ya ushindi kuelekea...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI benchi la ufundi la Yanga likisema limejipanga kuwashangaza US Monastir kutoka Tunisia, mabosi wa klabu hiyo wameweka wazi fedha za hamasa zinazotolewa na Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, zimeongeza ari kwa wachezaji wa timu hiyo katika kupambana kusaka ushindi.

Yanga inatarajia kuwakaribisha US Monastir katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Matokeo ya ushindi ndio yataongeza matumaini ya Yanga yenye pointi saba kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema kimbinu timu yao inaendelea vizuri na kila mchezaji anaelekezwa namna ya kutimiza majukumu yake kwa ufasaha katika mechi hiyo muhimu kwao.

Kaze alisema anaamini wachezaji wakitimiza vyema majukumu yao, timu hiyo itazibakisha pointi tatu nyumbani na kuwashangaza wapinzani hao.

Alisema katika mechi ya kwanza walifanya makosa wachache ambayo yaliwagharimu na kubababisha kufungwa mabao mawili ya haraka lakini tayari wameyafanyia kazi na sasa wanaandaa timu itakayowaduwaza Waarabu hao.

"Hatuwaogopi licha ya kufahamu wapinzani wetu wana timu nzuri, walitufunga kwao na sisi tuna uwezo wa kuwafunga hapa Tanzania, tunaendelea kujipanga ili tushinde na naamini tutafanya hivyo kama kila kitu kitaenda kama tulivyopanga," alisema Kaze.

Aliongeza morali ya wachezaji wao iko juu na kilichobakia ni kusubiri muda wa mapambano ambao wamejipanga kucheza kwa umakini ili wasonge mbele katika mashindano hayo.

Mrundi huyo alisema mechi ya Jumapili ni muhimu na inatoa uamuzi wa hatima ya kutinga hatua ya robo fainali huku mpinzani wao na vinara wa Kundi D, US Monastir yenye pointi 10 wakiwa tayari wameshasonga mbele.

Wakati huo huo, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia gazeti hili kila mchezaji wa timu hiyo ana ndoto ya kucheza robo fainali na kwa sababu hiyo wamejipanga kucheza kwa kiwango cha juu.

Saleh alisema kipindi cha nyuma timu yao ilikuwa inatolewa katika hatua ya awali ya michuano hiyo ya kimataifa, lakini sasa wana wachezaji wenye uzoefu na ambao wako tayari kuipigania nembo ya Yanga.

"Sisi kwa sasa tunashukuru kwa hamasa hii kutoka kwa Rais Samia, unawaona kabisa wachezaji wanavyopambana ili kuipatia timu matokeo mazuri, tunashukuru kwa kila kitu kinachochangia ushindi wetu.

"Historia imebadilika na wakati huu tunaenda katika mechi ya mwisho wa wiki tukiwa na shauku kubwa ya kuona timu yetu inashinda mbele ya wageni wetu US Monastir," kiongozi huyo alisema.

Baada ya mechi hiyo, Yanga itasafiri

INAENDELEA UK. 23



Nyota wa Yanga, Stephanie Aziz Ki.
**PICHA: MTANDAO**

## Simba yakamilisha hesabu za Horoya

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amesema anatarajia kufanya mabadiliko ya kiufundi kwa kuingia na mkakati mpya katika mechi ya Kundi C ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Simba itawakaribisha Horoya AC kutoka Guinea ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mechi mbili mfululizo za kimataifa dhidi ya Vipers FC ya Uganda na moja ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa ugenini iliwatandika wenyeji, Mtibwa Sugar mabao 3-0.

Robertinho aliliambia gazeti hili kikosi chake kinafahamu kina kazi kubwa ya kusaka ushindi katika mchezo huo kwa sababu wanakutana na timu ngumu.

Kocha huyo alisema mashindano ambayo wanashiriki si mepesi lakini wamejipanga kuvuna matokeo mazuri.

"Wachezaji ambao tunao wengi wana vipaji na uzoefu wa kupambana kutafuta matokeo bora, hakuna ambaye hatambui ubora wa wapinzani wetu (Horoya), lakini ni lazima tuwe na mpango kwa ajili ya kuwakabili.

Tunapaswa kuwabadilishia mipango kulingana na namna ambavyo tutakutana nao, tukiwa katika mazoezi ndipo tunafanyia kazi makosa yetu," alisema Robertinho.

Aliongeza kila mchezo wanaocheza wanaingia na mpango kazi maalum wenye lengo la kupata ushindi kwa kuzitumia vizuri nafasi za kufunga zinazopatikana na kujihakikisha kuzibakisha pointi tatu.

"Tulipoteza nchini Guinea na Horoya AC, kwa wapinzani wetu kutumia makosa yetu na kufanikiwa kufunga bao 1-0, ninaimani hayawezi kujirudia baada ya kuwepo na mpango na mkakati wa kupata ushindi na kucheza hatua ya robo fainali," alisema Robertinho.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002